

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Hamsini – Tarehe 13 Juni, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Tukae.

Katibu!

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 424

**Hitaji la Wodi ya Mama na Mtoto – Hospitali ya
Wilaya ya Lushoto**

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI aliuliza:-

Wilaya ya Lushoto ina hospitali moja ya Wilaya ambayo inabeba mzingo mkubwa sana wa watu. Aidha, wodi ya wajawazito ni chumba kidogo sana na hakuna kabisa wodi ya mama na mtoto.

Je, ni lini Serikali itajenga vyumba hivyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Hospitali ya Wilaya ya Lushoto bado ina changamoto ya msongamano katika wodi za akina mama wajawazito kwa sababu haina eneo la kutosha kukidhi wingi wa akina mama wajawazito wanaohudumiwa. Wodi ya akina mama wajawazito iliyopo imetokana na uamuzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kubadilisha matumizi ya baadhi ya majengo ili yatumike kama wodi ambapo jumla ya shilingi milioni 30 zilitumika katika mwaka wa fedha 2016/2017 kutengeneza wodi tatu ndogo ndogo yaani wodi ya akina mama wajawazito kabla ya kujifungua, wodi ya akina mama wajawazito baada ya kujifungua yenye uwezo wa kuhudumia akina mama sita kwa wakati mmoja, chumba cha upasuaji chenye vitanda vitatu vya upasuaji na wodi ya akina mama na watoto wachanga baada ya kujifungua kwa kawaida au upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kukabiliana na changamoto hiyo, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepeleka shilingi milioni 400 katika Kituo cha Afya cha Mlalo; shilingi milioni 500 katika Kituo cha Afya cha Mnazi na shilingi milioni mia tano katika Kituo cha Afya cha Kangagae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa matumizi ya fedha hizo ni kujenga vyumba vya upasuaji, wodi za mama na mtoto kabla na baada ya kujifungua na maabara kwa lengo la kuboresha huduma kwa mama wajawazito ikiwemo huduma za dharura za upasuaji kwenye maeneo hayo, hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa msongamano kwenye Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa wodi ya kisasa ya wajawazito (*maternity complex*) ni miongoni mwa vipaumbele vya juu vya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ndiyo maana katika mwaka wa fedha 2018/2019 imetenga shilingi milioni 25 kuanzisha ujenzi unaotarajiwa kukamilika mwaka 2019/2020.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri. Pia nashukuru kwa kuona hilo kwamba kweli Hospitali ya Wilaya ya Lushoto ina msongamano mkubwa sana.

Je, Serikali haioni sasa kuwa ipo haja ya kumalizia vituo vya afya vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi ambavyo ni Ngwelo, Makanya ambayo ni zahanati inayotakiwa ipandishwe hadhi iwe kituo cha afya, pamoja na Gare ili kupunguza msongamano uliopo katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa *x-ray machine* iliyopo katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto haina uwezo mkubwa wa kuhudumia watu wengi na hivyo kuzidiwa na kuharibika mara kwa mara na wagonjwa kukosa huduma hiyo muhimu; je, ni lini Serikali itapeleka *x-ray machine* ya kidijitali katika Hospitali ya Wilaya ya Lushoto na kupunguza usumbufu uliosababishwa na ubovu wa mashine hiyo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shekilindi katika swali lake la kwanza kuhusu kumalizia maboma kwenye vituo vya afya vitatu kikiwemo kimoja ambacho wanataka kukipandisha hadhi; nimwambie tu kwamba Serikali inaunga mkono. Mimi naomba sana katika fedha za ruzuku ambazo tutazipeleka

hivi karibuni, Halmashauri iweke kipaumbele kikubwa kwenye hivyo vituo ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *x-ray*, naomba tuendelee na mawasiliano, mwaka wa fedha mpya unaoanza ili angalau ifikapo mwezi wa kumi tuwe tumeshafanya maendeleo mazuri kwenye upande wa *x-ray*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kutokana na swali namba 424.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Kijiji cha Chiwale na tulifanya pale uzinduzi wa jengo la mama na mtoto, lakini hata hivyo, Kituo cha Afya cha Chiwale tulipewa ahadi ya gari ambayo hatujajua itatekelezwa lini na sasa hivi kile kituo kimekuwa kikubwa na kinahudumia watu wengi sana wa kata zile kwa sababu Jimbo la Ndanda lina Kituo cha Afya kimoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri: Je, ni nini mpango wao wa kuweza kutusaidia pale kuweza kupata angalau *mobile x-ray* ili kuwasaidia watu wa jirani? Kwa sababu kwenye Kata zote 16 tuna kituo cha afya kimoja tu, kwa hiyo, ni safari ndefu sana kutoka Chiwale kwenda Masasi kwa ajili ya kwenda kupata huduma za afya kwenye Hospitali ya Wilaya ilipo sasa hivi na wenyewe *x-ray* yao ni mbovu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwambe amezungumza mambo mawili ndani ya swali moja; amezungumzia ahadi ya gari la wagonjwa; nimwambie kwamba tuendelee na mawasiliano ya karibu ili kusudi hiyo ahadi iweze kutekelezwa, kwa sababu nia ya Serikali ni kutekeleza ahadi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili hili la *x-ray*, na mimi nimwombe sana kwamba pamoja na kuweka kipaumbele cha Halmashauri kwenye bajeti zake kwa mwaka ujao wa fedha katika fedha za ruzuku ambazo mwaka ujao zitapatikana mapema zaidi, kama zisipotosha, basi naomba tuwe na mawasiliano ya karibu na ofisi yetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hongoli.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, lina vituo vya afya vinne na kati ya vituo hivyo tumeanza kutoa huduma ya *theater* kwenye kituo kimoja cha Lupembe kwa kupitia fedha za ndani lakini pia michango ya wananchi na Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo mengine kwenye kituo hiki na kituo kimojawapo ambacho tumeomba cha Kichiwa, kiweze kupata huduma ya *theater* na kukamilisha majengo yale ya Lupembe kwa kuwa tumeomba muda mrefu na hatujapata fedha yoyote? Tumekosa shilingi milioni 500, tumekosa shilingi milioni 400 na vituo vyote hivi havina hata gari la wagonjwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi. Ajiandae Mheshimiwa Grace.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukamilisha majengo, Serikali inatambua kwamba yapo majengo mengi sana ambayo yameanzishwa kwa nguvu za wananchi na vilevile kwa uwezo wa Halmashauri na bado hayajakamilika. Nazidi kutoa wito kwamba naomba sana Halmashauri zote nchini ziweke kipaumbele cha kwanza kabisa kumaliza majengo ambayo yameanzishwa. Pale ambapo fedha yoyote ya ruzuku au fedha ya ndani inapokuwa imepatikana, basi waweke

kipaumbele sana kukamilisha majengo. Kuhusu gari la wagonjwa naomba tuendelee kuwasiliana na ofisi yetu ili tuweze kukamilisha kazi hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Grace, baada ya hapo tunaendelea.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro imekuwa kwenye ujenzi wa wodi ya wazazi zaidi ya miaka mitano sasa na wodi hiyo haijakamilika na kusababisha gharama za ujenzi kuongezeka. Je, ni lini Serikali itatoa pesa za kutosha kukamilisha wodi hiyo ya wazazi? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, napenda nitoe ahadi kwamba tutawasiliana ndani ya Serikali ili tuweze kutimiza matarajio ya Mheshimiwa Mbunge katika Hospitali ya Mkoa wa Kilimanjaro.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu sahihi. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, Wizara hiyo hiyo na Ofisi hiyo hiyo.

Na. 425

Hitaji la Kituo cha Afya – Mwese

MHE. ANNA R. LUPEMBE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Mwese?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu. Hongera kwa swali la Kibunge. Hili ndiyo swali la Kibunge. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 7 Mei, 2018, Serikali ilipeleka jumla ya shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujenga chumba cha mionzi (*x-ray*), nyumba ya mtumishi, maabara, chumba cha upasuaji, wodi ya mama na mtoto na chumba cha kuhifadha maiti kwenye Kituo cha Afya cha Mwese katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda. Ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2018.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lupembe.

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niipongeze Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanya kusema kweli kwa hiki kituo, kilikuwa ni kituo chakavu sana na kinatumika na watu wengi sana. Tunashukuru sana kwa hizi pesa ambazo mmetuletea na kuanzia sasa hivi ukarabati umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wafanyakazi wa sekta hii ni wachache sana, hatuna kabisa manesi, madaktari wala wahudumu kabisa; je, ni lini Serikali itatuletea watumishi katika kituo hiki ha Mwese? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Hospitali ya Manispaa ya Mpanda ndiyo hospitali inayobeba matatizo yote katika Mkoa wetu wa Katavi; je, ni lini Serikali itatuletea Madaktari Bingwa, kwa sababu Hospitali ya Mpanda haina Madaktari Bingwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, ajiandae Mheshimiwa Kakoso.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nipokee pongezi zake kwa fedha ambazo tumepeleka Mwese na nimpongeze naye mwenyewe kwa kufanya kazi za Kibunge hasa katika Mkoa wake wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la watumishi katika Kituo cha Mwese, napenda nimhakikishie kwamba kwa sababu kituo hakijakamilika, Serikali itaweka kipaumbele katika kutenga watumishi ambapo kituo hicho mara kitakapokamailika tu tutawapeleka mara moja ili waweze kutoa huduma kwa wananchi. Hao watumishi tutawaajiri mwezi Julai, wataanza kazi, wataripoti, lakini kuna watumishi ambao tutawa-*retain* kwa ajili tu ya Kituo hiki cha Mwese.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupeleka Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Manispaa ya Mpanda, kwanza nilitembelea hospitali ile mwezi Novemba, 2017 hospitali yenyewe tu kwanza inahitaji uangalizi wa karibu kwa maana ya ukarabati na mambo mengine. Nimhakikishie kwamba katika ajira ambazo tunaendelea nazo sasa hivi, kati yetu sisi tuna ajira 6,000 ambazo tunaendelea kuziratibu na Wizara ya Afya ina ajira kati ya 1,800 mpaka 2,000 ambazo wanaendelea kuziratibu, basi tutaweka kipaumbele cha kupeleka Madaktari Bingwa kupitia ajira hizi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Shangazi na Mheshimiwa Julius Kalanga.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza naishukuru na kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa wanayoifanya baada ya kutoa fedha za kupeleka Kituo cha Afya cha Mwese na Kituo cha Afya cha Mishamo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jiografia ya Jimbo la Mpanda Vijijini ambalo lipo katika Wilaya ya Tanganyika liko katika mazingira ya mtawanyiko; je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka *ambulance* ambayo itawasaidia kwenye

hivyo vituo vya afya; Kituo cha Afya cha Karema, Kituo cha Afya cha Mwese na Kituo cha Afya cha Mishamo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kutokana na eneo mtawanyiko mkubwa wa Jimbo la Mpanda Vijijini lililopo katika Wilaya ya Tanganyika ambayo ni Wilaya mpya kunahitajika *ambulance* kutokana na kwamba maeneo yako mbalimbali sana; Mwese, Mishamo na kile kituo kingine ambacho amekitaja. Tutakapopata mgao wa *ambulance* ambao utapatikana kabla ya mwezi wa kumi, basi naomba sana tuendelee na mawasiliano ya karibu ili tumpe kipaumbele.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Lushoto yenye tarafa tano ina Vituo vya Afya katika Tarafa ya Mlola, Mlalo, Mnazi pamoja na Lushoto Mjini; je, ni lini sasa Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Tarafa pekee iliyobaki ya Mtae?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ya maswali yote ya awali. Mheshimiwa Shangazi alishafika ofisini kwetu mara kadhaa kuhusu kituo hiki na ndiyo maana tumeanza katika awamu hii kupeleka pale Mnazi. Naomba nimhakikishie kwa sababu wananchi wa Mtae wanapata shida, katika kipindi kinachokuja tutafanya kila liwezekanalo, kuhakikisha eneo lile tunalipatia Kituo cha Afya. Lengo letu ni kupunguza vifo vya mama na watoto. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Julius halafu Mheshimiwa Kawambwa ajiandae.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika ziara ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI mwezi Machi, 2017 katika Halmashauri ya Monduli aliahidi kusaidia juhudi za wananchi katika Kituo cha Afya cha Makuyuni. Pamoja na hayo, katika mwaka wa fedha 2017/2018 fedha zote za ruzuku tulielekeza katika ujenzi wa Vituo vya Afya.

Je, ni lini Serikali italeta fedha za *CDG* katika Halmashauri ya Monduli kwa ajili ya kumalizia Vituo vya Afya Lemuoti, Nalarani, Makuyuni pamoja na Duka Bovu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Mheshimiwa Julius Kalanga awe na mawasiliano ya karibu na Mkurugenzi wa Halmashauri kwa sababu wakati wowote fedha za ruzuku zinaweza zikaingia. Sasa zikiingia waweke kipaumbele kwenye hayo maeneo.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu. Waheshimiwa Wabunge tuna Mheshimiwa Kawambwa.

MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Jimbo la Bagamoyo kata zake zote isipokuwa moja tu ndiyo ina kituo cha afya ambacho ni kipya. Je, ni nini mpango wa Serikali kuweza kutupatia angalau kituo kimoja au viwili zaidi kwa Jimbo zima la Bagamoyo? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli

Wilaya ya Bagamoyo ina changamoto kubwa na hivi sasa tuliimarisha katika Kituo cha Afya cha Kerege. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kadri iwezekanavyo na tukijua kwamba jioografia ya Bagamoyo na mahitaji yake yalivyo, nadhani kabla hatujafika mwezi wa saba, hapa katikati, tutafanya jambo katika kituo kimoja cha afya ambacho yatapendekeza kutoka Wilaya ya Bagamoyo. (Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini.

Na. 426

Kupandisha Hadhi Zahanati ya Migungumalo kuwa Kituo cha Afya

MHE. ALMAS A. MAIGE aliuliza:-

Zahanati ya Migungumalo, Kata ya Usagari Uyui ilijengwa kwa maandalizi ya kuwa Kituo cha Afya na kufunguliwa na Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa tarehe 25/11/1997 na kuahidi kuwa zahanati hiyo itakuwa Kituo cha Afya cha Kanda ya Magharibi.

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kuikuza zahanati hiyo ili iwe Kituo cha Afya kutokana na mahitaji na huduma zinazotolewa kuwa juu ya uwezo wa zahanati?

(b) Kwa kuenzi kazi na juhudi za Rais Mstaafu Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kufika mpaka Usagari kufungua zahanati; je, Waziri yuko tayari kumwomba Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano kuja kuzindua Kituo cha Afya baada ya kuipandisha hadhi Zahanati hiyo ya Migungumano?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Zahanati ya Migungumalo inahudumia wananchi na inatoa huduma za kiwango cha juu. Zahanati hii imeendelea kutengewa fedha kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa wananchi kupitia Mfuko wa Pamoja wa Afya, fedha za matumizi mengineyo, fedha za Benki ya Dunia (*RBF*), Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*) na fedha za dawa kupitia Bohari ya Dawa (*MSD*). Lengo la Serikali ni kuendelea kuiwezesha zahanati hiyo iendelee kutoa huduma nzuri zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, miundombinu iliyopo kwa sasa katika Zahanati ya Migungumalo haikidhi vigezo vya kutoa huduma za afya kwa ngazi ya kituo cha afya. Kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kujenga vituo vipya na kuboresha vituo vya afya vilivyopo nchi nzima ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wagonjwa zikiwemo huduma za dharura na upasuaji.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali inaendelea na ujenzi wa vituo cha afya 210 kikiwemo Kituo cha Afya cha Upuge ambacho kimepokea shilingi milioni 500 ili kukiwezesha kutoa huduma za dharura na upasuaji. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Tabora/Uyui imetengewa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ambayo ikikamilika itahudumia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Serikali ya Wilaya, Halmashauri na viongozi wa Kata ya Usagari ili waanze juhudi za kujenga Kituo cha Afya cha Kata ya Usagari na ikiwezekana waanze juhudi za kujenga zahanati katika kila kijiji kama sera ya afya inavyoelekeza. Serikali iko tayari kuunga mkono nguvu za wananchi katika kumaliza ujenzi huo utakaofanyika chini

ya uratibu wa halmashauri, ofisi ya Mbunge na ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Kuja kwa Mheshimiwa Rais au kiongozi mwingine wa kitaifa itategemea sana na aina ya miradi itakayokamilika. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige.

MHE. ALMAS. A MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza sana Serikali kwa fedha ambazo imetupatia kwa ajili ya Kituo cha Upuge na fedha ambazo zinapelekwa kwenye zahanati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo naomba niseme ukweli kwamba methali ya kwamba mzigo mzito mpe Mnyamwezi, hatuitaki tena kwa sababu inatukandamiza. Tunasema mzigo mzito punguza, beba mwenyewe. Kwa sababu tumegundua kwamba kumbe mzigo mzito ni kutokuwa na vituo vya afya, kutokuwa na barabara huko kwetu, hatutaki tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunataka Bunge hili lielewe kwamba Wilaya yote ya Uyui ina kituo kimoja tu cha afya, sidhani kama kuna Wilaya nyingine hapa Tanzania iko namna hiyo, lakini vilevile hakuna tena hospitali ya Wilaya katika Wilaya nzima. Kwa hiyo, vituo vya afya vilivyopo, zahanati hizi ndiyo tunazomba zipanuliwe ziweze kuwa vituo vya afya. Kwa hiyo, wananchi wa Kata ya Usagari, wamechanga shilingi milioni 50 wakiwa na lengo la kupanua kituo kile kiwe kituo cha afya na maeneo yapo. Tunaona ni bora kungezeza kuliko kujenga upya...

MWENYEKITI: Mheshimiwa swali.

MHE. ALMAS. A MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, je, Serikali iko tayari kubadili msimamo wake ili hela za wananchi, shilingi milioni 50 na Mfuko wa Jimbo wa shilingi milioni 10 watuongezee tupanue kituo kile kiwe kituo cha afya? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

MHE. ALMAS. A MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, samani swali langu la pili.

MWENYEKITI: La pili, haya.

MHE. ALMAS. A MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; kwa kujua hali ilivyo kule Jimboni kwangu kwamba hakuna kituo cha afya, hakuna zahanati bora zaidi ya hiyo ya Migungumalo; je, Serikali iko tayari kutusaidia kujenga kupandisha Zahanati za Ilonguru na Ufuluma ili vitumike kwa muda kama vituo vya afya?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, mhusika.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la mtani wangu Mnyamwezi wa Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata maombi yake Mheshimiwa Maige. Hata hivyo naomba nikiri wazi kwamba Mbunge huyu amekuwa mpiganaji sana wa eneo lake. Hata siyo muda kwa kazi kubwa anayofanya, hata jina la Halmashauri yake muda si mrefu sana litabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba kutokana na changamoto, ndiyo maana tuliwapa fedha kuimarisha Kituo cha Afya cha Upuge ambacho sasa hivi kinaenda vizuri, lakini hata katika bajeti ya mwaka 2018/2019 kutokana na shida kubwa waliyokuwa nayo tumewapa takriban shilingi bilioni 1.5 watajenga Hospitali ya Wilaya. Vilevile kabla ya tarehe 15 mwezi wa saba katika Jimbo la Igalula tutapeleka fedha nyingine kwa ajili kuimarisha kituo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba wananchi wa jimboni kwako tutafanya kila liwezekanalo ili kama kuna vituo ambavyo vinatakiwa tuvipe hadhi, tutaangalia nini tufanye, lengo letu kubwa kama Serikali ni kuhakikisha kwamba Wanyamwezi

wa Tabora wanapata huduma ya afya vizuri kama wengine.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mwalongo.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa naishukuru Serikali kwa kutupatia fedha milioni mia tano kujenga Kituo cha Afya cha lhalula, lakini naomba kuiuliza Serikali; je, lini sasa watatupatia fedha kwa ajili kukarabati Hospitali ya Halmashauri ya Mji Njombe Kibena?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mwalongo kwa sababu juzi nilienda kukagua kituo kile wamejenga vizuri sana. Nilipokuwa Mkoani Njombe nilitembelea vituo mbalimbali, miongoni mwa kituo ambacho wametumia taaluma vizuri ya *Force Account*, Mheshimiwa Mwalongo mmefanya vizuri. Hata hivyo tunafahamu katika ujenzi, hasa changamoto ya miundombinu, kama Serikali, tunachukua hili tunaweka katika mipango yetu. Lengo kubwa ni kwamba isiwe kwa hospitali yako peke yake, lakini hospitali mbalimbali za Wilaya ambazo zinachangamoto lazima tulirekebishe ili wananchi wapate huduma vizuri. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hawa Ghasia, ajiandae Mheshimiwa Qambalo.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naipongeza sana Serikali katika kuhakikisha inaboresha miundombinu ya sekta ya afya. Hata hivyo, je, Serikali iko tayari kwenda sambamba na uongezaji wa watumishi katika maeneo hayo? Kwa sababu sasa hivi changamoto kubwa sana ni watumishi katika zahanati zetu na vituo vya afya pamoja na hospitali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikia Mheshimiwa Hawa Ghasia, ninafahamu kwamba siyo muda mrefu tutaimarisha kituo chake cha Mahulunga pale katika Jimbo lake ambalo najua kwamba changamoto ya watumishi itakuwa kubwa. kwa bahati nzuri Naibu Waziri alishasema awali kwamba tunaajiri watumishi 6,180.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawapa kipaumbele katika miundombinu hii wananchi waweze kupata huduma ya afya katika Jimbo la *Mtwara DC*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Qambalo, ajiandae Mheshimiwa Neema.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kituo cha Afya Endabash katika Tarafa ya Endabash inahudumia kata nne, lakini kituo hicho kina upungufu mkubwa ikiwemo jengo la mama na mtoto, maabara na *mortuary*. Ni lini Serikali itatoa fedha ili miundombinu hiyo iliyobaki ikamilike ili kituo hicho kioe huduma stahiki?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Endabash ni sehemu yenye changamoto kubwa. Tukijua wazi kwamba Wilaya yetu ya Karatu ni *center* kubwa ya watalii, ndiyo maana katika mipango mikakati yetu kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI tunataka kuangalia tuone ni jinsi gani tutafanya tu *upgrade* kituo kimoja. Mimi naamini kwamba kwa sababu ya ajenda kubwa ya utalii, jukumu langu kubwa ni kuhakikisha unajipanga vizuri na watu wako, ikifika kabla ya mwezi Disemba kituo hicho kiwe kimekamilika kwa ajili ya kuwatumikiwa wananchi wa eneo hilo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Neema. Halafu tunaendelea.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Wanging'ombe kuna Kituo cha Afya cha Makoga. Kituo hiki ni cha kimkakati, kinahudumia wananchi wa Tarafa ya Imalinyi na Mdandu. Tuseme ni theluthi mbili ya wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe wanapata huduma katika Kituo cha Afya hicho cha Makoga, lakini hali yake ya miundombinu ni mibaya sana. Je, ni lini Serikali itatoa pesa ili kuweza kukarabati Kituo kile cha Afya cha Makoga?

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Waziri, kubwa lao. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Neema Mgaya na Wabunge wa Njombe wote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwepo kule tukifanya harambee na tulipata shilingi milioni mia moja na thelathini na saba. Namshukuru Mheshimiwa Neema, Mheshimiwa Lwenge na Waheshimiwa Wabunge wote. Hii tulifanyia pale Makoga na kweli changamoto yake ni kubwa. Hata hivyo tulitembelea Kituo kingine cha Afya cha Palangawano ambacho kinajengwa. Kwa hiyo, kama Serikali tumeweka kipaumbele katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabla ya mwezi wa 12 kati ya vituo hivyo viwili tutaweza kukiboresha kituo kimojawapo. Hata hivyo *priority* ya Makoga na Palangawale lazima tuikamilishe kwa ajili ya wananchi wa Wanging'ombe waweze kupata huduma vizuri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maji na umwagiliaji, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

Na. 427

Tatizo la Maji - Jimbo la Ukonga

MHE. LUCY S. MAGERELI (K.n.y. MHE. MWITA M. WAITARA) aliuliza:-

Jimbo la Ukonga katika Kata za Msongola, Chanika, Zingiziwa, Buyuni na Pugu kuna shida kubwa sana ya maji.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu wa kuondoa kero ya maji katika kata hizo?

(b) Je, ni lini miradi viporo vya maji na visima vyenye pampu mbovu vitafanyiwa matengenezo ili kupunguza kero ya maji Ukonga?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara Mbunge wa Jimbo la Ukonga lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa muda mrefu wa kuondoa kero ya maji katika Jiji la Dar es Salam na viunga vyake kwa kutumia maji ya visima virefu 20 vilivyochimbwa katika Manispaa ya Kigamboni eneo la Kimbiji na Mpera vyenye uwezo wa kutoa kiasi cha maji cha mita za ujazo 350 mpaka 700 kila kimoja. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza maji katika maeneo hayo. Kukamilika kwa mradi huu kutaondoa kero ya maji katika Jiji la Dar es Salam na viunga vyake zikiwemo Kata za Msongola, Chanika, Zingiziwa Buyuni na Pugu. Mradi huu unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2018/2019.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu ya Pili ya Utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP //) Serikali imeweka kipaumbele cha kukamilisha miradi viporo

kabla ya kuanza miradi mingine mipya. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepanga kukamilisha miradi viporo na kukarabati visima vyenye pampu mbovu kwa kutumia fedha za Mpango wa Malipo kwa Matokeo (*Payment by Result*). Mpaka sasa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala imekarabati na kumalizia ujenzi wa miradi viporo sita ya maji katika Jimbo la Ukonga kwenye Kata za Msongola, Pugu, Mzinga na Pugu Stesheni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Magereli.

MHE. LUCY S.MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na nimeshukuru kupata majibu ya Serikali, lakini...

MWENYEKITI:... ajiandae Mheshimiwa Lubeleje.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijauliza maswali yangu mawili ya nyongeza naomba nitoe maelezo mafupi ya utangulizi kwamba ni fedheha na ni mambo ya aibu kabisa kwa Jiji kongwe kama Dar es Salam kwa Mji Mkuu wa biashara wa muda mrefu tangu uhuru wa nchi hii kupatikana kuendelea kuteseka na adha ya maji mpaka leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Serikali anazungumzia habari ya visima 20 ambavyo vinachimbwa Mpera na Kimbiji. Kwa bahati mbaya ni kwamba visima hivyo mpaka sasa havijakamilika kwenye zoezi la kuchimbwa.

Je, fedha wanazosema wanatafuta, zinatafutwa kutoka wapi na zitapatikana lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwenye majibu ya Waziri anasema katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imepanga kukamilisha miradi ya viporo kama kipaumbele. Tunavyozungumza bajeti 2017/2018 inakwisha siku chache sana zijazo na bado....

MWENYEKITI: Swali, uliza swali.

MHE. LUCY S. MAGERELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swala hili linaitwa kipaumbele.

Je, Mheshimiwa Waziri anajibu tofauti kwenye swali (b)?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu anasema unapaswa kushukuru kwa kila jambo na usipowashukuru binadamu hata Mwenyezi Mungu unaweza hutamshukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kabisa Jiji la Dar es Salam lilikuwa na changamoto kubwa sana ya maji, lakini mpaka sasa asilimia 78 ya wananchi wanapata maji safi, salama na yenye kuwatosheleza. Watu wa Mamlaka ya *DAWASCO* wana mpango mkubwa mkubwa wa kuongeza mtambo ile wa Ruvu juu na Ruvu chini katika kuhakikisha wananchi wa Dar es Salaam wanaendelea kupata maji, safi salama na yenye kuwatosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa katika maeneo ya viunga vya Dar es Salam kwenye changamoto ya maji Serikali imeshachimba visima 20 na sasa tumejipanga katika kuhakikisha tunasambaza maji ili wananchi wa Ukonga na maeneo mengine waweze kupata maji safi, salama na yenye kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya viporo, kazi inaendelea kufanyika, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aendeleo kutuamini na sisi katika yale maeneo ambapo tunahitajika kukamilisha viporo vile tutaendelea kuvikamilisha kwa wakati, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Mariam Kisangi.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Nina swali moja tu la nyongeza; kwa kuwa maji ni siasa, maji ni uchumi, na maji ni maendeleo; na kwa kuwa Serikali ilikuwa na mipango ya kuchimba visima vya maji katika Kijiji cha Majami, Nana, Mafuto, Lupeta 30, Makutupa pamoja na Ngalamilo na walielezwa kabisa fedha zilizotengwa kwa ajili ya visima hivyo.

Je, ni lini sasa Serikali watakwenda kuanza kuchimba visima vya maji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Wizara yetu ya Maji ni katika kuhakikisha wananchi wanapata maji safi, salama. Nimuombe sana Mheshimiwa Mbunge mimi kama Naibu Waziri wa Maji nipo tayari kufanya *cross check* na watu wa *DDCA* waende mara moja katika kuhakikisha wananchi wake wa Mpwapwa wanapata safi, salama na yenye kuwatosheleza, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mariam Kisangi, ajiandae Dkt. Kikwembe.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa maboresho makubwa ya miradi ya maji katika Jiji la Dar es Salam. Kwa kweli katika maeneo ya Masaki, Oysterbey, Tabata, Segerea, masuala la maji yalikuwa magumu mno, sasa hivi Oysterbey, Masaki wanapata maji hawanunui kwenye maboza, ni jambo kubwa naipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nakiri kwamba bado kuna maeneo yana changamoto ya maji ikiwemo hilo Jimbo la Ukonga pamoja na maeneo ya Mbande, Chamanzi,

Majimatitu, Mianzini, Kiburugwa, Mbagala Kuu, Kibondemaji na Kilungule, huko bado kuna matatizo ya maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kuyasaidia maeneo hayo wakati tukisubiri visima vya Mpera?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri muhusika.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe taarifa na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba tumepata fedha shilingi bilioni hamsini na saba kutoka Benki ya Dunia na tumeshatangaza *tendertayari* kwa ajili ya kuendelea kusambaza maji katika Jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Jiji la Dar es Salaam tutahakikisha tunakamilisha maji yanapatikana katika maeneo yote.

MWENYEKITI: Ahsante ameshakuelewa, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ajiandae Mheshimiwa Kubenea.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ina mpango wa kurekebisha na kuvitibu visima viporo ambavyo mpaka leo havijatengenezwa.

Je, Serikali inasema nini sasa kuhusu visima vyangu virefu ambavyo vimetengenezwa miaka sita iliyopita mpaka leo havijarekebisha, ambavyo ni, Kisima cha Tupindo, kilichopo Kata ya Mbede na Kisima cha Kibaoni ambavyo mashine zake zimedumbukia ndani na vimetumia kutengezwa takribani pesa za Serikali milioni 800?

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, Waheshimiwa leo tuna azimio.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kazi kubwa inayofanywa na mama yangu Kikwembe. Nimuombe tu kwa kuwa Wahandisi wote wapo bado Dodoma, labla baada ya saa saba afike na Mwandisi wake ili tuangalie namna gani tunaweza tukamsadi katika kutatua tatizo la maji.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru. Kwa kuwa tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam limekuwa kubwa, katika Majimbo karibu yote ya Jiji la Dar es Salaam; na kwa kuwa Serikali imekuwa inasema Bungeni karibu miaka mitano sasa kwamba imepata fedha kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha mfumo wa maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Je, ni lini hasa mradi huu wa Benki ya Dunia utaanza rasmi katika Jiji la Dar es Salaam?

MWENYEKITI: Mheshimiwa majibu ni lini, Waziri muhusika.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza mwaka ujao wa fedha kwa sababu tayari tumeshatangaza *tender*.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri; kwa sababu Jimbo la Sumve lina visima 89 ambavyo ni vibovu havitoi maji, na barua unayo; je, ni lini visima hivyo sasa vitatengenezwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu lini.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:
Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Ajiandae Mheshimiwa Ritta Kabati.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua changamoto hizo na viporo mbalimbali Waziri wangu akaona haja sasa kwa Wabunge wote kupitisha barua kuangalia namna gani na kuorodhesha maeneo ambayo yenye changamoto. Labla nimuombe Mheshimiwa Mbunge jambo hili baada ya kulichukua tutalifanyia kazi kwa wakati na yeye katika maeneo yake hatomuacha katika kuhakikisha tunamrekebisha visima vyake, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ritta Kabati, tunaendelea Wizara zingine baadae.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa swali dogo la nyongeza. Nimpongeze kwanza Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kuja katika Mkoa wetu wa Iringa na kujionea jinsi ambavyo Mji wetu wa Iringa ulivyokua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuuliza swali dogo; kwa kuwa Mji wa Iringa unakua kwa kasi kubwa sana, kuna baadhi ya maeneo ambayo hayapati maji kama kule Tagamenda, Isakalilo na Kigonzi. Je, Serikali ina mpango gani wa kutuletea pesa ili kuongeza ule mtambo wa kusambaza maji pamoja na kuwa sasa hivi tunapata asilimia 96, lakini maji yetu tunaweza tukapata asilimia 100?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu, Waziri mhusika.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama cha Mapinduzi wakati inajenga mtambo wa kutibu maji Iringa iliweka matoleo ili *population* itakapoongezeka basi tuweze kupanua ili maji yaweze kuongezeka. Katika mwaka ujao wa fedha tumetenga bajeti kwa ajili ya kuanza kupanua mtambo wa kutibu maji ili maji yaweze kuenea katika kata zote.

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea, tuna Azimio leo, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Kapufi.

Na. 428

Fedha kwa Ajili ya Uzazi wa Mpango

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI aliuliza:-

Mahitaji halisi ya fedha kwa ajili ya uzazi wa mpango kwa mwaka kwa sasa ni zaidi ya shilingi bilioni 36 katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga shilingi bilioni 14.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha zaidi ili kufikia kiasi kinachohitajika pia kuongeza kasi ya kuokoa maisha ya akina mama na watoto chini ya umri wa miaka mitano?

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa makisio halisi ya bajeti kwa ajili ya uzazi wa mpango nchini ni shilingi bilioni 36 na kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imetengwa shilingi bilioni 14. Hata hivyo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa shilingi bilioni 14 zilizotengwa ni sawa na ongezeko la asilimia 50 zaidi ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017 ambazo zilikuwa shilingi bilioni saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa za uzazi wa mpango pamoja na dawa zingine muhimu kwa kufuata taratibu maalum za mpango wa manunuzi. Kwa sasa dawa za uzazi

wa mpango zinapatikana katika ngazi zote kuanzia Bohari Kuu ya Dawa hadi kwenye vituo vyote vya kutolea za afya vilivyopo Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeweka mkakati maalum kwenye Mikoa na ya Simiyu, Geita, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Kigoma na Katavi ambako matumizi ya uzazi wa mpango yako chini ya wastani wa kitaifa wa asilimia 32 kwa wanawake walio kwenye ndoa. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 22.5 kwa ajili ya uzazi wa mpango kutoka katika vyanzo vya ndani. Kiwango hiki cha fedha ni sawa na ongezeko la asilimia 60 kutoka mwaka 2017/2018.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mpango wa maendeleo ya vitu, kwa mgano, ujenzi wa shule, visima na kadhalika ni watoto pacha na mpango wa uzazi. Serikali inasema nini katika kuhakikisha haiishii kutenga fedha bali fedha zionekane zikipelekwa eneo hilo la uzazi wa mpango?

Swali la pili, mimba za utotoni ni janga la Taifa, Mkoa wangu wa Katavi tunaongoza kwa maana ya asilimia 45. Serikali inasema nini katika kushirikiana na wananchi wa Mkoa wa Katavi ili kuwanusuru wananchi wale na janga hili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Kapufi kwamba upo uhusiano wa moja kwa moja wa maendeleo na ongezeko la idadi ya watu na Serikali imeliona suala hili na ndiyo maana pia katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, suala la uzazi wa mpango na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango amekuwa kisitiza huduma za uzazi wa mpango na ndiyo

maana ukiangalia tumetoka asilimia 27 mwaka 2012 sasa hivi ni asilimia 32. Kwa hiyo fedha zinatoka za Serikali na tumeamua kabisa kutumia fedha zetu za ndani badala ya kutumia fedha za wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni mimba za utotoni, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba ni changamoto. Asilimia 27 ya watoto wa kike wamepata ujauzito kabla hawajatimiza umri wa miaka 18, kwa hiyo, katika mpango wetu wa kuzuia mimba za utotoni *especially* katika Mkoa ya Katavi tumeamua kutumia njia za kuwaelimisha wasichana wajizuie kuingia katika vitendo vya ngono mpaka pale watakapofikisha umri wa miaka 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa kweli hali siyo nzuri, watoto wetu wa kike wanaanza ngono, asilimia 14 ya watoto wakike wanaanza ngono kabla hawajafikisha umri wa miaka 15 na watoto wa kiume ni asilimia tisa. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mtusaidie katika kuhamasisha na kuelimisha wasichana hasa kujizuia kufanya mapenzi kabla hawajatimiza umri wa utu uzima. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Masoud, ajiandae Mheshimiwa Issaay.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa uzazi salama haujafanikiwa ipasavyo kwani kunakuwepo na upungufu mkubwa wa Madaktari, wauguzi na wakunga katika vituo vingi vya afya hasa huko vijijini.

Serikali ituambie ina mpango gani mkakati wa ziada kuhakikisha kwamba mnapeleka madaktari, wakunga na wauguzi katika vituo vya afya na zahanati katika maeneo ya vijijini zaidi ili kuokoa maisha ya akina mama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala la uzazi salama linategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa rasilimali watu wenye sifa na ujuzi, lakini asilimia 64 kwa mujibu wa utafiti wetu sasa hivi ya wanawake wanajifungua katika vituo vya afya na wanahudumiwa na wataalam wenye ujuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nakiri kwamba zipo changamoto, Mheshimiwa Jafo ameeleza pale Serikali itaajiri watumishi wa afya 6,000 kupitia TAMISEMI na watumishi wa afya 2,000 kupitia Wizara ya afya, lakini tumeenda mbali zaidi, tumepata fedha bilioni moja, tunasomesha watumishi wa afya 200 katika kutoa huduma za dawa za usingizi na tutawapeleka katika vituo vya afya ambavyo vinaboreshwa ili sasa pale ambapo wanawake watafanyiwa upasuaji kwa ajili ya huduma za dharura watapata huduma ambazo ni salama lakini pia zinazofikika kwa wanawake wengi zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Issaay, ajiandae Mheshimiwa Mabula.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kushukuru Serikali kwa kujenga vituo vya afya katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa ziara yake pamoja na muda huu wa mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani amejitahidi kwenda Mbulu na kuona changamoto zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Halmashauri ya Mji wa Mbulu ina Tarafa tatu; Tarafa ya Nambis katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu haina hata kituo kimoja cha afya. Changamoto kubwa inayowakabili wakina mama wa Tarafa ya Nambis katika hali ya kupata huduma ya uzazi salama. Je, ni lini sasa Serikali itatupa fedha na ahadi ya Mheshimiwa Waziri ya kwenda kwenye ile Tarafa ya Nambis ambako wananchi wengi na hasa akina mama wanapata tatizo kwenye uzazi?

MWENYEKITI: Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge *please*. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Issaay kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini kwa kweli kazi yako inaonekana na imetukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la kupata kituo cha afya katika Kata ambayo haina Kituo cha afya tumeshirikiana na wenzetu wa TAMISEMI tayari kuna mpango wa kuhakikisha kwamba kata ambazo hazina vituo vya afya zinakuwa na vituo vya afya na vijiji ambavyo havina zahanati vinakuwa na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba nitumie Bunge lako tukufu kutoa angalizo, sera ya afya inasema kituo cha afya kila kata na zahanati kila kijiji, lakini tunafanya mapitio ya sera ya afya. Tutatoa vigezo kwamba kituo cha afya kila Kata kwa kuzingatia jioografia ya eneo husika, idadi ya watu na *burden of disease* (aina ya magonjwa ambayo yanapatikana katika eneo hili) kwa sababu sasa hivi barabara nzuri lakini pia kuna mawasiliano ya simu.

Kwa hiyo, sitaki kuwadanganya Wabunge kwamba tutakuwa na vituo vya afya kila kata, haitawezekana. Tutaweka vigezo ili tuone ni kata zipi ambazo zitakuwa na vituo vya afya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mabula.

MHE. STANLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa swali la nyongeza.

Naomba tu kuuliza; kwa kuwa uzazi wa mpango ni moja ya mkakati madhubuti kabisa wa kuzuia vifo vya mama na watoto na nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwamba kwa mpango ujao Mkoa wa Mwanza ni moja ya Mikoa iliyowekewa mikakati, lakini Wilaya ya Nyamagana ni

moja ya Wilaya zinazoongoza kwa vifo hivi vya Mama na mototo kwenye Mkoa wa Mwanza. Ni nini sasa mkakati madhubuti kwa ajili ya Nyamagana ili kuhakikisha vifo vya Mama na mototo vinakwisha kabisa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mabula na hasa ukiona wanaume wanazungumzia suala la uzazi wa mpango maana yake tunatoka. Tutaongeza idadi ya wanawake wanaotumia njia za kisasa za uzazi wa mpango lakini nampongeza kwa kazi nzuri Nyamagana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza tusipochukua hatua madhubuti, mwaka 2030 Tanzania itakuwa na watu milioni 70 na haiendani na ukuaji wa uchumi na itakapofika 2050 tutakuwa na Watanzania milioni 100 ambapo hatuoni pia ikilingana na ongezeko la uchumi. Kwa hiyo, tumeamua kuja na mkakati wa kuhimiza wanawake hasa walio kwenye ndoa, naomba niliseme hili, wanawake walio kwenye ndoa hutumia huduma za uzazi wa mpango na asilimia 39 ya wanawake walio kwenye ndoa wameeleza kwamba wanapenda kuchelewa kupata watoto kwa kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nirudie, kwa Mheshimiwa Mabula tunaanzisha vituo vya kutoa huduma za uzazi wa mpango katika miji kwa sababu suala la uzazi wa mpango siyo ugonjwa. Wanawake wa Dar es Salaam, wanawake wa Nyamagana hawataki kwenda hospitali kupanga foleni kwa ajili ya kupata huduma. Kwa hiyo, tutawafuata akina mama ambao wanauza mboga mboga...

MWENYEKITI: Ahsante.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: ...tutakuwa na *mobile clinic*. Kwa hiyo,

mama akitaka huduma anapata palebadala ya kupanga foleni masaa mawili, masaa matatu na tunawashukuru sana wadau wetu wa maendeleo ambao wametusaikia kuhakikisha huduma hizi za uzazi wa mpango Mijini pamoja na Nyamagana zinapatikana kwa urahisi.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu mazuri. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, muda wetu umekwenda na leo tuna Azimio.

Na. 429

Hitaji la Ofisi ya Wilaya ya Kipolisi Mbalizi

MHE. ORAN M. NJEZA aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini wanaipongeza Serikali kwa kuanzisha Wilaya ya Kipolisi Mbalizi.

(a) Je, ni lini Ofisi ya Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi pamoja na nyumba za askari zitajengwa?

(b) Je, Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi ina magari mangapi na Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya vituo vya polisi katika Halmashauri ya Wilaya Mbeya?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi ni miongoni mwa Wilaya Mpya za Kipolisi zilizoanzishwa hivi karibuni. Jeshi la Polisi kwa kutambua ukosefu wa Ofisi ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya pamoja na nyumba za makazi ya askari linashirikiana na wananchi na wadau mbalimbali kujenga jengo la Ofisi ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya ambalo linajumuisha Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo hili umefikia hatua ya umaliziaji na changamoto iliyobaki ni ujenzi wa nyumba za kuishi askari.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi ina magari matatu ambapo gari moja ni chakavu linahitaji matengenezo ili liweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya vituo vya Polisi katika Halmashauri ya Mbeya pamoja na kwingineko nchini kwa awamu kwa kutegemea rasilimali zilizopo na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Njeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwanza nianze kabisa kuipongeza Serikali pamoja na changamoto zote hizi za miundombinu na idadi ndogo ya askari lakini bado wameimarisha ulinzi katika Wilaya ya Mbeya na hususani Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi.

Swali la kwanza, je, ni lini Serikali itapeleka shilingi milioni 120 ambazo zitaunga mkono shilingi milioni 200 walizotumia wananchi kukamilisha Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kipolisi ya Mbalizi?

Swali la pili; je, ni lini Serikali itajenga Vituo vya Polisi katika miji inayochipukia ya Mjele, Ilembo pamoja na Igoma? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika umaliziaji pamoja na majengo mapya aliyoyasemea tutaweka kipaumbele katika mwaka huu wa fedha pamoja na bajeti zitakazofuatia kulingana na upatikanaji wa rasilimali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze tu Mheshimiwa Mbunge, amefanya jitihada kubwa sana katika jengo hili

ambalo tunalisemea na aendeleo na moyo huo huo na ndiyo maana wananchi wa Mbalizi pamoja na Mbeya Vijijini wanaendelea kumuamini na kuchangua.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kafumu, Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Devotha Minja.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Wilaya ya Igunga ina Kata 35 na ina Vituo vya Polisi saba, Kituo cha Igunga, Nanga, Ziba, Simbo, Sungwizi na Choma na Igurubi lakini ina magari mawili tu ya polisi. Nauliza ni lini Serikali itasaidia Wilaya ya Igunga ikapata magari mengi ili kuhudumia wananchi wetu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi anataka kujua ni lini tu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Kafumu kwa kulileta swali ambalo linaungwa mkono na jiografia ya Wilaya ya Igunga na naitambua Wilaya ya Igunga na natambua umuhimu wa swali alilouliza Mheshimiwa Kafumu, niseme tu tutaweka uzito pale tutakapokuwa tunagawa vitendea kazi kulingana na upatikanaji wake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Jimbo la Mtama alikuta tunajenga Kituo cha Polisi pale Mtama na akaahidi kwamba tukimaliza ujenzi wa kile kituo atatupatia gari kwa ajili ya kusaidia huduma za usalama katika lile eneo. Ni lini sasa ahadi hii ya Waziri Mkuu itatekelezwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ahadi lini, ajiandae Mheshimiwa Devotha Minja.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Nape kwa ufuatiliaji wake wa masuala ya jimboni kwake. Niseme tu kwamba ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni maelekezo na sisi tutafanyia kazi maelekezo hayo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Devotha Minja, jandae Mheshimiwa Mgumba.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kumezuka tabia mbaya ya Jeshi la Polisi, wanapokwenda kumkamata mtuhumiwa wakimkosa wanakamata mtu mbadala akiwa mke au watoto.

Naomba kufahamu Jeshi la Polisi linatoa wapi mamlaka haya ambapo wanashindwa kutumia mbinu zao za kiintelijensia kukamata mtuhumiwa badala yake wanarahisisha na kukamata mke au watoto na kuwatesa?

MWENYEKITI: Swali hilo lingine kabisa lakini lijibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Devotha Minja, shemeji yangu na niseme tu kwa Jeshi la Polisi linafanya kazi kwa mujibu wa sheria na niseme hakuna mtu anayeruhusiwa kufanya adhabu kwa mbadala. Kosa linabaki kuwa la mkosaji. Kwa hiyo, nielekeze tu popote pale ambapo pana mtu amefanya kosa atafutwe yule yule aliyekosa na kama wengine wanaweza wakasaidia basi wasaidie katika namna ya kuelezea jinsi wanavyoweza kufahamu, lakini siyo kuchukua adhabu ya mtu mwingine aliyekosa.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mgumba.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kipaumbele cha watu wa Kinole ni ujenzi wa Kituo cha Polisi ambacho tumeshajenga ambacho kimefikia mtambaa wa panya kinasubiri kuzekwa pamoja na ujenzi wa kituo cha afya; na kwa kuwa katika Kata ya Kinole kuna SACCOSS ya mfano yenye mtaji wa zaidi ya shilingi bilioni mbili na wakulima wakubwa wa matunda na viungo lakini kuna mzunguko mkubwa sana wa pesa lakini usalama ni mdogo na Serikali imepeleka pesa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Kisimbi.

Je, Serikali iko tayari kuhamisha pesa hizi ilizopeleka katika ujenzi wa Kisimbi ambao ni ujenzi wa kituo cha utalii ambao siyo kipaumbele cha wananchi na kuna tatizo la mgogoro wa fidia na kupeleka kwenye umaliziaji wa Kituo cha Polisi kwenye mapato ya ndani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo alilolisema Mheshimiwa Mbunge ni pendekezo. Niseme tu kama Serikali tunapokea pendekezo, lakini nimuombe Mheshimiwa Mbunge tupate fursa tuongee kwa undani zaidi ili tuweze kuhusisha na wadau wengine na Wizara zingine ambazo zinahusika.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Susan Lyimo.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kabla sijauliza swali langu ninaomba kutoa pole nyingi sana kwa Profesa Anangisye, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Jumuiya nzima ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kupotelewa na wanafunzi wawili, muuguzi na dereva baada ya *ambulance* ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam kupata ajali usiku wa kuamkia juzi.

Na. 430

Utekelezaji wa sera ya Elimu Bure kwa Vitendo

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Sera ya elimu ya mwaka 2014 inatambua elimu ya msingi kuwa ya lazima bila malipo.

Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge hili na Taifa kwa ujumla ni lini ulazima huu utatekelezwa kwa vitendo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza naomba vilevile nipokee pole za Mheshimiwa Mbunge na nitazifikisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, lakini Wizara vilevile imezipokea.

Mheshimiwa Mweyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka utaratibu wa elimu ya msingi kuwa ya lazima na kuweka kipaumbele cha kuhakikisha kuwa kuna fursa sawa ya kupata elimu kwa ngazi hii yaani elimu ya awali, msingi na sekondari hadi kidato cha nne. Kwa sababu hii ndiyo ngazi ya elimu ambayo humpatia mhusika stadi za msingi za kuweza kukabiliana na mazingira yake. Dhana ya elimu bila malipo inazingatia uendeshaji wa shule bila ada wala michango ya aina yoyote ya lazima kutoka kwa wazazi au walezi wa wanafunzi na hivyo kuondoa vikwazo vya uandikishaji na mahudhurio ya watoto shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa sasa utekelezaji wa elimu ya msingi ya lazima ni kwa muda wa miaka saba

kama inavyoelekeza Sheria ya Elimu iliyopo yaani Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 Sura ya 353.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa elimu msingi kuwa ya lazima kwa vitendo tangu mwaka 2015/2016 kwa kufidia gharama za uendeshaji wa shule za umma ambapo hupeleka fedha moja kwa moja shuleni kama fidia ya ada, na fedha za rukuzu ya uendeshaji wa shule yaani *capitations grands*. Serikali pia hupeleka fedha kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wa bweni wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mpango huo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ongezeko la uandikishaji na kuimarika kwa mahudhurio ya wanafunzi darasani. Aidha Serikali inafanya jitihada za kukabiliana na changamoto zilizojitokeza kama vile mahitaji ya vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, maabara, madawati, walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuhakikisha kuwa elimu inatolewa kwa ubora unaotakiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lyimo.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ni kweli ule msembo ukishangaa ya Musa utaona ya firau, ukishangaa ya Musa utaona ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaweza kutuambia kwamba ilitudanganya kwa sera hii kwa sababu ilisema elimu msingi ni darasa la kwanza mpaka la sita. Leo wanasema elimu ya msingi ni darasa la kwanza mpaka la saba kwa sheria ya mwaka 1978. Sasa wako tayari kuwaambia wananchi kwamba sasa wanafunzi watakuwa wanasoma darasa la kwanza mpaka la saba na kwamba ile sera ilikuwa ya kutudanganya? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa sasa wamekiri kwamba elimu msingi kwa maana ya elimu ya awali mpaka kidato cha nne haiwezekaniki, tena na sasa ni elimu ya msingi ya darasa la kwanza mpaka la saba.

Sasa nataka kujua hiyo, mitaala ambayo tayari walishaihuisha ya kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la sita kwa maana ya kwamba la saba lilikuwa halipo, wataenda tena kukaa na kutunga mingine au watafanyaje? Nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba Serikali imedanganya kwa kubadilisha elimu msingi kuwa miaka saba badala ya ile sita iliyokuwa imesemekana katika sera ya elimu ya mwaka 2014, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hakuna kosa lililofanyika kwa sababu sera ni njozi, ni vitu ambavyo unatarajia kufanya katika kipindi cha muda mrefu, kwa hiyo, hakuna ulazima wa kufuata sera kwa asilimia 100. Kitu ambacho ni lazima kufuata ni sheria na Sheria yetu ya Elimu ya mwaka 1978 mpaka leo hii ndio sheria ambayo inatuongoza na ndio inatutaka tufuate elimu msingi ya miaka saba bila kukosa.

Kwa hiyo, kama tunataka tuhakikishe ile miaka sita inakuwa kisheria hatuna budi kubadilisha sheria na ndio kazi hasa ya Bunge hili. Kwa hiyo, kama yeye anaona kwamba ni lazima kufanya hivyo aje na mapendekezo na sisi hatuna shida.

Lakini niseme vilevile kwamba waingereza wanasema *don't fix that which is not broken*, hatujaona shida na elimu ya miaka saba katika shule ya msingi. Waheshimiwa wote mlioko huku wote mmesoma katika mfumo huo. Kuhusu kwamba tulishapendekeza busara ikijua nyingine wakati wowote ili mradi ni kitu kizuri haina shida, hakuna kosa lililofanyika na tutaendelea kwa miaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la mitalaa, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kurekebisha mitaala yetu ili tuendane na maamuzi yoyote ambayo tutakuwa tumechukua kwa wakati huo. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah.

Na.431

Mgogoro Kati ya Wananchi wa Kihurumile na Hifadhi ya Selous

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH aliuliza:-

Mgogoro wa ardhi katika Hifadhi ya Wanyamapori Selous-Kilwa umechukua nafasi kubwa kati ya Serikali na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hiyo. Mpaka halali haujulikani kwani mwaka 1974 mpaka halali ulikuwa Mto Matandu na mwaka 2010 mpaka huo ulisongezwa mpaka Bwawa la Kilurumila, Kijiji cha Kikulyungu.

Je, Serikali ipo tayari kuhakiki eneo hilo ili kutatua mgogoro uliopo kati yake na wananchi wa Kijiji cha Kihurumile?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Abdallah Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kijiji cha Kikulyungu ni moja ya vijiji tisa vinavyopakana na Pori la Akiba la Selous kwa Wilaya ya Liwale. Ndani ya pori hilo kuna bwawa lijulikanalo kama Kihurumila ambalo ni sehemu muhimu kwa mazalia ya samaki na wanyamapori kama vile mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka 1970 wananchi wa Kijiji cha Kikulyungu walikuwa wakivua samaki katika bwawa hilo baada ya kupewa vibali maalum. Hata hivyo, mwaka 1982 Serikali ilizuia shughuli za uvuvi kutokana na baadhi ya wananchi kukiuka taratibu za kuvua samaki ikiwemo matumizi ya sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka wa Pori la Akiba Selous umewekwa kwa kuzingatia Tangazo la Serikali Na. 275 la mwaka 1974. Tangu wakati huo hadi sasa mpaka huo haujafanyiwa marekebisho yoyote. Hata hivyo, wananchi wa Kijiji cha Kikulyungu hawakubaliani na tafsiri na uhakiki wa mpaka uliofanyika licha ya vijiji vinne kukubaliana na uhakiki huo. Aidha, wananchi wa Kijiji cha Kikulyungu wanadai kwamba Bwawa la Kihurumila ni sehemu ya eneo la kijiji hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilituma maafisa kuhakiki mipaka ya vijiji vitano kati ya vijiji tisa vinavyounda *WMA* ya Liwale vinavyopakana na Pori la Akiba la Selous. Vijiji hivyo ni Kimambi, Kikulyungu, Barikiwa, Chimbuko na Ndapata. Uhakiki huo ulishirikisha pia Maafisa kutoka Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi Tanzania, Maafisa Ardhi Wilaya ya Liwale, Taasisi isiyo ya Kiserikali ijulikanayo kama *World Wide Fund for Nature (WWF)* na wananchi na Viongozi wa Kata na Vijiji vinavyounda Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Liwale. Zoezi hili lililenga kutatua mgogoro wa mpaka na kutangaza *WMA* ya Liwale. Hata hivyo, wananchi wa Kikulyungu waliwafanyia vurugu watalaam wa Wizara ya Ardhi walipotembelea eneo la mgogoro kwa ajili ya kutafsiri Tangazo la Serikali na kusababisha watalaam kukimbia kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia hali hiyo, Wizara imepanga kukutana na viongozi wa Mkoa wa Lindi akiwemo Mheshimiwa Mbunge kwa lengo la kutatua mgogoro huo kwa manufaa ya uhifadhi na ustawi wa wananchi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamida.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu haya ambayo ameyatoa japokuwa hayaoneshi dhamira ya dhati ya kutaka kumaliza mgogoro huo. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza, mgogoro huu umekuwa wa muda mrefu sana, lakini kwa majibu ya Serikali hayakuonesha hapa ni lini watakutana na viongozi wa Mkoa ili kumaliza huu mgogoro. Kwa sababu umesema tu watakaa lakini haisemi ni lini. Kwa sababu huu mgogoro ni wa muda mrefu kwa hiyo, ningepomba Serikali ituambie ni lini watadhamiria kumaliza huu mgogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali langu la pili, kuna mgogoro pia kwenye Serikali ya Wilaya ya Kilwa na Wizara kuhusiana na mpaka huu wa Selous. Kwa hiyo, nayo Mheshimiwa Waziri ningependa aniambie ni lini mgogoro huu watamaliza ili kuepokana na vurugu ambazo zinaweza zikatokea katika kugombania mipaka hii katika maeneo haya?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu, swali lake ni lini tu mnakutana.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hi kumpongeza sana kwa sababu amekuwa ni mdau mzuri sana wa mambo ya utalii katika eneo la kusini, kwa kweli tutaendelea kushirikiana naye. Sasa kuhusu lini tutakutana naomba nimhakikishie tu kwamba kati ya mwezi wa saba na wa tisa kabla ya Bunge la mwezi tisa tutafanya jitihada za kuhakikisha kwamba tunakutana na viongozi wa Lindi na tutashughulikia migogoro yote inayohusiana na hilo Pori la Akiba la Selous.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Chikambo, Mheshimiwa Kuchauka.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini naomba niulize swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo migogoro inayoendelea baina ya vijiji vyetu na hifadhi zetu, ikiwemo Hifadhi hiyo ya Selous ambayo muuliza swali ameizungumza, lakini pia ipo

migogoro baina ya kijiji na kijiji, hii inapelekea wananchi wengi kukosa amani.

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kumaliza migogoro hii katika nchi yetu ili wananchi waendeleo kuishi kwa amani? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kumekuwa na changamoto, kumekuwa na migogoro mbalimbali katika maeneo mbalimbali yanayopakana na hifadhi. Lakini naomba nitumie nafasi hii kumueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 yaani Julai, Wizara kwa kushirikiana na taasisi zetu za Hifadhi za Taifa tutahakikisha kwamba vijiji vyote vinavyozunguka maeneo ya hifadhi vinapimiwa na vinaondokana na matatizo ambayo yapo katika yale maeneo. Kwa sababu tumetenga fedha kwa ajili ya hiyo kazi kwa hiyo vijiji vyote vitapitiwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka, ajiandae Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Waziri kwamba, ndiyo vinavyochangia katika Wilaya ya Liwale kwa Selous, vijiji hivi ndivyo vilivyoanzisha mgogoro kwa sababu vijiji hivi vimepakana na Selous kwa Mto wa Matandu. Kwa nini Kikulyungu peke yake ndio ambayo imeonekana kwamba imeondoka Matandu na ndio maana wanakijiji Wakikulyungu waligoma. Sasa Mheshimiwa Waziri ninachotaka kujua je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kufuatana na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi muende mkatafsiri GN ambayo inaitambua Pori la Akiba la Selous ukiachana na hii tangazo la mwaka 1974?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba tuko tayari kuongozana na Mheshimiwa Waziri pamoja na viongozi wengine wa Mkoa wa Lindi ili tushughulikie migogoro yote inayohusu mpaka wetu kule. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri pale Segerea kuna pori moja linaitwa Msitu wa Nyuki, walikuwa wanafuga nyuki zamani lakini naona Wizara imeshaachana na huo mpango wa kufuga nyuki.

Sasa Wizara ina mpango gani na hilo pori maana yake wameliacha tu, na kama hawana mpango nalo kwa nini wasitupe sisi Manispaa ya Ilala ili tuweze kuitumia katika matumizi ya soko na mambo mengine ya huduma za kijamii? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba tuna msitu katika lile eneo ambalo lilikuwa linatumika kwa ajili ya kufuga nyuki, lakini si kwamba lile pori tumeliacha tu, kuliacha tu bado linaendelea kuhifadhi ule uoto wa asili.

Kwa hiyo, bado ni pori linalotambulika vizuri kabisa na bado tutaendeleza jitihada za kufuga, lakini pia inasaidia sana katika kuweza kupunguza *carbon dioxide* ambayo inatokea katika viwanda mbalimbali pale Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lile eneo tutaendelea kulihifadhi na litaendelea kuhifadhi na kuendelezwa.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo.

Na. 432

Uendelezaji wa Sekta ya Mifugo

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA aliuliza:-

Asilimia 95 ya eneo lote la Wilaya ya Longido hutumika kwa ufugaji wa wanyamapori. Aidha, asilimia tano ya eneo hilo ndiyo hutumika kwa shughuli za kilimo.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza sekta ya mifugo kwa kuzingatia kuwa mifugo ndio shughuli kuu ya uchumi wa wananchi wa Longido na Wilaya nyingine za ufugaji nchini?

(b) Je, ni lini Serikali itapatia Hati ya Idhini ya kutumia na kusimamia (*User Rights Certificate*) Jumuiya ya Uhifadhi wa Wanyama Pori (*WMA*) wa Kanda ya *Lake Natron*?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Mbunge wa Longido lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeandaa mkakati wa kuboresha sekta ya mifugo nchini unaolenga kuongeza tija na uwekezaji katika mifugo, kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali yatokanayo na biashara ya mifugo na mazao yake ili kuongeza mchango wa mifugo katika Pato la Taifa. Aidha, mikakati ya kuendeleza sekta ya mifugo katika Wilaya ya Longido inahusisha ujenzi wa mnada wa kimkakati wa Eworendeke ambao umekamilika na unatarajiwa kuzinduliwa rasmi Julai, 2018. Mnada huu utasaidia wafugaji kupata soko la uhakika la mifugo. Pia, Halmashauri ya Longido imepata mwekezaji ambaye atajenga kiwanda cha kusindika nyama katika eneo la Eworendeke ambacho kinatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Wilaya ya Longido kuwa na Hali ya Ukame Halmashauri imejenga mabwawa, vibanio vya kunyweshea mifugo pamoja na kusambaza madume bora ya ng'ombe kwa lengo la kuboresha mifugo ya asili ilikupata mifugo bora inayostahimili mazingira ya Longido na kukua kwa haraka. Pia Halmashauri itaendelea kutoa huduma za ugani kwa wafugaji kwa lengo la kuboresha ufugaji ikiwamo kutoa mafunzo kuhusu mabadiliko ya tabia ya nchi na uboreshaji wa maeneo ya malisho.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Ziwa Natron ni pori tengefu kwa mujibu wa Kanuni za Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) za mwaka 2012 kifungu cha 8(1)(a)-(c). Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori huanzishwa katika maeneo yaliyo nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kisheria. Aidha, hati ya matumizi ya rasilimali za wanyama pori kwa maana ya *User Rights Certificate* hutolewa kwa Jumuiya ya Hifadhi za Wanyama pori iliyoanzishwa na kusajiliwa kisheria. Kwa kuwa eneo hilo bado ni Pori Tengefu, limeendelea kupangiwa vitalu vya uwindaji wa kitalii ambapo wananchi na Halmashauri ya Wilaya wananufaika na asilimia 25 ya mapato yatokanayo na ada za wanyamapori wanaowinda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Steven.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza na kabla sijauliza maswali yangu kwanza nipende kumpongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuinua sekta ya mifugo. Lakini hasa niishukuru Serikali kwa ajili ya soko hilo lililojengwa kule mpakani mwa Kenya na Tanzania katika Kijiji cha Eworendeke, na nitoe rai kwamba waachiwe halmashauri waendeshe kwa sababu ndio waliobuni Wizara itoe tu *oversight*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza kwa kuwa jamii hii ya kifugaji ili mifugo iwalettee tija wanahitaji malisho, maji, tiba ya chanjo na kutibu magonjwa

sambamba na masoko ya uhakika na ninashukuru kwamba soko la Eworendeke linaweza kuja kuwa soko la uhakika waondokane na adha ya kupeleka mifugo huko nje ya nchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutusaidia hasa wafugaji wa *West Kilimanjaro* waweze kupata hayo maeneo ya kulishia hasa ukizingatia kuna mgogoro mkubwa ambao umekuwa ukitokea kila wakati wa kiangazi kwenye yale mashamba pori yaliyotelekezwa na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili linamhusu Waziri wa Maliasili kwa sababu maswali yangu yalichanganywa, kwa sababu nililiza swali moja kwa ajili ya Wizara ya Utalii na majibu niliyopata sikuridhika nayo. Eneo lote la Wilaya ya Longido ni Pori Tengefu na dhana ya *WMA* ilipoanza mchakato ulifuatwa *WMA* ndiyo ikapatikana. Mchakato ukapitiwa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swali.

MHE.DKT. STEVEN KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *WMA* ya *Lake Natron* imepitia mchakato wote. Ni kwa nini *WMA* hii haitangazwi na imebakia kutangazwa tu na kitu kinawezekana?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mbunge huyu mpya kwa kazi kubwa nzuri anayoifanya ya kuwasimamia wafugaji wa eneo hili la Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anataka kwanza, Mheshimiwa Mbunge namna ambayo tutakavyoweza kushirikiana nao kama Halmashauri, nataka nimhakikishie ya kwamba sisi kama Wizara tutawapa ushirikiano na hatutafanya kazi ile ya usimamizi wa moja kwa moja isipokuwa tutakuwa pale kwa pamoja kuhakikisha kwamba kodi zote za Serikali ambazo zinasimamiwa na Wizara zitakuwa zinapatikana kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya suala la *West Kilimanjaro*, naomba nimhakikishie na niwahakikishie wafugaji wote wa eneo lile, ikiwa ni pamoja na Longido, Siha na kwingineko ya kwamba mkakati wetu mahususi wa Wizara ni kuhakikisha kwamba wafugaji ng'ombe hawafi tena. Wakati maeneo ya asili ambayo yanamilikiwa na Wizara yetu kwa maana ya ranchi ziko pale. Tumekuballana ya kwamba wafugaji watapewa ruksa ya kupewa vitalu katika maeneo yale anaingiza ng'ombe wake, ng'ombe mmoja kwa kiasi cha shilingi 10,000; anamlisha, anamnyweshwa katika ranchi ile kwa muda wa miezi mitatu ananepa na kumtoa kumpeleka sokoni.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kiruswa na wafugaji wote nchini ya kwamba tumejipanga vyema na tutawasaidia katika jambo hilo.

MWENYEKITI: Ahsante, Waheshimiwa tuna Mheshimiwa Waziri wa Maliasili

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa majibu mazuri aliyotoa.

Kuhusu hili suala la *WMA* kutangazwa katika lile eneo naomba kwanza niweke vizuri tu kwamba *WMA* ni hatua ya kwanza ya uhifadhi ambayo inashughulikiwa na vijiji vinavyozunguka maeneo ya hifadhi, baada ya hapo inakuja pori tengefu baada ya hapo pori la Akiba, baada ya hapo hifadhi ya Taifa. Sasa tumeshafika tayari kwenye pori tengefu hatuwezi kurudi tena chini kwenye *WMA*, lile eneo litaendelea bado kuwa ni pori tengefu, lakini baadae tutaangalia kama sifa zinaliruhusu kuwa ni pori la akiba baada ya hapo tutaendelea kupanda zaidi badala ya kurudi nyuma. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa muda wetu umekwisha na maswali yote ya msingi yamekwisha sasa ni matangazo ya wageni na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliopo Jukwaa la Spika wageni saba wa Mheshimiwa Spika (Mbunge) ambao ni viongozi wa UWT Taifa, Mheshimiwa *Comrade* Gaudentia Kabaka - Mwenyekiti UWT Taifa, Mheshimiwa *Comrade* Thuwayba Kisasi - Makamu Mwenyekiti UWT Taifa, Mheshimiwa Queen Mlozi - Katibu Mkuu Taifa, Mheshimiwa Eva Mwingizi - Naibu Katibu Mkuu Taifa, Mheshimiwa Grace Kingalame - Mjumbe Baraza Kuu UWT Taifa, Mheshimiwa Neema Majule - Mwenyekiti UWT Dodoma na Mheshimiwa Christina Dominic - Msaidizi wa Katibu Mkuu UWT Taifa. *(Makofi/Vigelegele)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni saba wa Mheshimiwa Wabunge *Engineer* Isack Kamwelwe (Mbunge) Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea mkoani Katavi. *(Makofi)*

Wageni 43 wa Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye - Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ambao ni Madiwani 17, Makatibu Kata CCM Jimbo la Muhambwe 23 na viongozi watatu wa CCM Wilaya ya Kibondo wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kibondo Ndugu Hamisi Tahiro, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Jumaa Aweso Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji ambao ni wapiga kura wake toka jimboni kwake Pangani Mkoani Tanga, karibuni wageni wa Waziri Mheshimiwa Aweso. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mussa Ntimizi ambao ni viongozi wa *Universal Peace Federation* kutoka nchini Senegal wakiongozwa na Katibu Mkuu wa *UPF Africa* Ndugu Adam Duombia, *welcome to the Parliament.* *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaye ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM kutoka Wilaya ya Kilolo Mkoani Iringa Ndugu Said Kiponza. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Joshua Nassari ambaye ni mpiga kura wake kutoka Mkoani Arusha Ndugu Simon Moshia,

karibu. Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa George Lubeleje ambaye ni Mheshimiwa Olgene John - Diwani kutoka Jimboni kwake Mpwapwa Mkoni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambaye ni familia yake kutoka Dar es Salaam, karibuni. Pia kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni ndugu zake kutoka jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 66 na walimu kumi kutoka shule ya msingi Angelico Lipani kutoka Jijini Arusha, karibuni Dodoma. Pia kuna wanafunzi 50 na walimu watano kutoka shule ya msingi *Mount Kibo* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 15 ambao ni waumini na wachungaji kutoka Kanisa la KKKT Ushirika wa Malanduku Mkoani Njombe, karibuni Dodoma. Wanafunzi 96 na walimu wanne kutoka shule ya msingi Martin Luther ya hapa jijini Dodoma wakiongozwa na mwalimu Mkuu wao mwalimu Gilbert Nhuguti, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lucy Magereli anaomba kutangaza kumtambulisha uwepo wa binti yake Maria Rhobi Magereli, karibu Dodoma. *(Makofi)*

Leo Jumatano tarehe 13 Juni, 2018 kutakuwa na Ibada ya Misa kwa Wakristu wakatoliki mara baada ya kuhairishwa Bunge katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili aidha Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki ibada hiyo. Tangazo hili limeletwa na Mwenyekiti wa Jumuiya Mheshimiwa Shally Raymond.

Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge anaomba kuwatangazia Wabunge wote kwamba katika bajeti ya miradi ya maendeleo ya Fungu 42, Mfuko wa Bunge kwa mwaka wa fedha 2017/2018 miongoni mwa shughuli zilizotengewa fedha ni ujenzi wa *lift* katika Jengo la Utawala

Annex pamoja na marekebisho ya paa la Jengo la Utawala, hivyo anawafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba kazi hiyo tayari zimeanza na kwa mantiki hiyo katika kipindi hiki kutakuwa na mafundi mbalimbali wanaoingia na kutokana na pirikapirika zinazohusiana na ujenzi huo.

Ofisi ya Spika inaomba kuwatangazia Wabunge wote na watumishi wote na wageni wote wanaopaki magari kwenye eneo la *parking* la Bunge kuwa kuanzia leo magari hayo yasiwekwe mpaka baada ya sikukuu kutokana na shughuli maalum ya futari inayoandaliwa kesho na Mheshimiwa Spika.

Kwa hiyo basi, wenye magari yote katika eneo la *parking* karibu na hospitali mpya yasiwekwe kuanzia leo ili maandalizi ya shughuli ya Mheshimiwa Spika ianze kuandaliwa.

Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu - Katibu wa Kamati ya Wabunge Wanawake CCM anaomba kuwatangazia kuwa Mheshimiwa Gaudentia Kabaka Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) anapenda kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wote wanawake pamoja na watumishi wa Bunge wanawake kwenye futari leo tarehe 13 Juni kuanzia saa 12 jioni kwenye viwanja vya Bunge Jengo la Utawala. (*Makofi*)

Mheshimiwa William Ngeleja Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge matokeo ya mechi iliyochezwa jana tarehe 12 Juni kwenye uwanja wa Jamhuri Dodoma *Bunge Sport Club (Ndugai Boys)* na *Bodaboda FC* timu ya Mheshimiwa Bonnah Kaluwa na matokeo ilikuwa timu ya Bodaboda ilifungwa magoli matatu kwa mawili. Nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Yussuf Kaiza, shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi waliojitokeza kushangilia timu hiyo. Katibu! (*Makofi*)

NDG. PAMELA PALLAGYO – KATIBU MEZANI:

AZIMIO LA BUNGE

Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Uamuzi wake wa Kuendeleza Mji wa Dodoma na Kuupa Hadhi ya Jiji

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mwongozo nitatoa miwili tu Mheshimiwa Susan na Mheshimiwa Dkt. Steven. Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu anajibu swali langu namba 430 pamoja na mambo mengine amesema kwamba mitaala itaendelea kuboreshwa. Ni kweli kwamba mitaala iliyopo sasa hivi imekuwa *condensed* au imehushwa kwa maana ya kwamba sasa mitaala ni ya kuanzia darasa la kwanza mpaka la sita. Lakini Mheshimiwa Waziri hapa amesema sasa tunafuata sheria ya mwaka 1978 ambapo elimu ya msingi kwa maana ile ya *primary* itakuwa darasa la kwanza mpaka la saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapooonea baada ya swali lile nimepata simu lakini hata wenye shule humu ndani wamenifuata wamepata mtafaruku kwa sababu hata mitihani ya darasa la nne tayari imeandaliwa kwa *syllabus* hii ya darasa la kwanza mpaka la sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu sasa kwa sababu ya mtafaruku huu nilikuwa naomba Mwongozo wako ili Wizara iweze ama kutoa waraka ama kueleza sasa wanaenda kutengua ile mitaala iliyokuwepo na nini sasa

kitaendelea kwa sababu kwa kweli imeleta matatizo makubwa sana katika elimu yetu. Ni hilo tu nilikuwa naomba sana Mwongozo wako ili tuweze kujua elimu inaendeshwa kwa namna gani? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Steven.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, wakati Waziri wa Maliasili na Utalii alipokuwa anajibu swali langu la msingi kipengele (b)alitoa majibu ambayo kwa kweli tusipoangalia tutaleta mtafaruku usio na lazima. Kwa sababu mchakato wa kuanzisha *WMA* ndani ya eneo la *Lake Natron* upande wa Longido ni miaka mingi takribani miaka nane mchakato ukiendelea na ni eneo ambalo wananchi walishahamasishwa wakagaramika. Wadau wa uhifadhi wakaingiza pesa nyingi mamilioni ya pesa na Wizara chini ya Idara ya Wanayamapori wakatoa ushirikiano wote. Mchakato ukafanyika wananchi wakafahamu kwamba lile eneo linawapa mamlaka ya kushirikia katika kulihifadhi na kupata fursa ya kufaidikia uhifadhi huo na wakawa wanangojea tu cheti. Halafu leo isemekane kwamba ni pori tengefu na hatuwezi kurudi nyuma na hiyo ukafikiri wananchi wa Longido wakisikia watakaa kimya nasikitika kwamba suala hili linahitaji Bunge lilijadili tulipatie muafaka. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante umeshaeleweka, ahsante Waheshimiwa miongozo yote nimeipokea na Waziri unataka kujibu Waziri wa Elimu mhusika, Mheshimiwa Naibu kaa.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kujibu Mwongozo ambao umeombwa na Mheshimiwa Susan Lyimo na Mwongozo wake unahusiana na mitaala ya elimu ya msingi.

Kwanza nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu vizuri kwamba elimu ya msingi ni miaka saba kama ambavyo imeanishwa katika Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 na kuhusiana na mitaala ambayo inatumika kwa sasa

Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri kwamba inaendelea kutumika mitaala kwa miaka saba. Kwa hiyo, hoja yake ya kwamba tufute tuandike waraka wa kufuta mitaala inayotumika. Hakuna waraka wowote ambao uliandikwa na kusema kwamba elimu itakuwa ni miaka sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna jambo lolote la kufuta kwa sababu elimu ni miaka saba na sheria haijabadilika inaonyesha kwamba elimu ni miaka saba. Kwa hiyo kama kuna mchanganyiko wowote ni mchanganyiko ambao mtu ameamua kujiwekea kichwani mwake mwenyewe kwa sababu hakuna waraka wowote ambao uliandikwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hakuna jambo lolote la kufuta kwa sababu utaratibu unafahamu, mabadiliko ya sheria yanafanywa ndani ya Bunge hili, Serikali haijawahi kuleta mapendekezo ya mabadiliko yoyote ya sheria. Nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa Waziri wa Uvuvi, Mheshimiwa Utalii na Waziri wa Uvuvi mko tayari kujibu au mnataka muda?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kidogo kuhusiana na hili eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameuliza. Tunachosema sisi ni kwamba yapo maeneo ambayo yanamilikiwa na Serikali za vijiji vinavyohusika. Sasa katika yale maeneo vile vijiji vinavyozunguka hifadhi kama yale maeneo yana umuhimu na kuna wanyamapori ambao wako maeneo jirani au wanapita katika yale maeneo tunavishauri vile vijiji viunde jumuiya ya kuhifadhi wanyamapori katika yale maeneo. Sasa tulichosema ni kwamba katika yale maeneo ambayo hayako kwenye pori tengefu yako nje ya pori tengefu yale maeneo yataendelea kuunda hii jumuiya na tutashirikiana Mheshimiwa Mbunge pamoja na viongozi wengine mpaka tutaizindua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lile eneo ambalo tayari ni pori tengefu hili hatatalimega kurudi kuwa chini ya Serikali

za vijiji kuwa kwenye jumuiya kwenye WMA hili litaendelea kuwa chini ya Serikali Kuu chini ya mamlaka ya usimamizi wa wanyamapori ambao ni TAWA. Kwa hiyo, ndio ufanunuzi ambao nilitaka kuusema kwamba yale maeneo ambayo yako nje ya hifadhi hayo tutakayounda hiyo jumuiya ya kusimamia wanayamapori.

MWENYEKITI: Ahsante mengine Dkt. Kiruswa unaweza ukakutana na Waziri mka-*caucus* mkapata muafaka. Katibu!

NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI

AZIMIO LA BUNGE

Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Uamuzi wake wa Kuendeleza Mji wa Dodoma na Kuupa Hadhi ya Jiji

MWENYEKITI: Azimio, Mheshimiwa Simbachawene.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya utangulizi kuhusu Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuendeleza Mji wa Dodoma kuupa hadhi ya Jiji.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. HALIMA J. MDEE: Kuhusu Utaratibu!

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Simbachawene subiri kidogo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene analeta hoja yake kwa mujibu wa kanuni ya 54 ya Bunge, lakini kanuni ya 56 inasema; Mbunge ambaye ataitwa wakati anatoa hoja kutokana na hiyo kanuni ya 54 anasimama mahali pake na kutoa hoja yake. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa Mheshimiwa Simbachawene arudi pale, aketi pale, alete hoja yake hapo mbele hapamuhusu kwa sasa *as far as* kanuni aliyoombea kutoa hoja. *(Makofi/ Kicheko)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Simbachawene endelea! *(Makofi/ Kicheko)*

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya utangulizi kuhusu Azimio la Bunge la kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wake wa kuendeleza Mji wa Dodoma na kuupa hadhi ya Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha azimio hili ambalo lengo lake kubwa ni kutambua na kuunga mkono juhudi kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli za kuendeleza mji wetu Mkuu wa Dodoma kwa kuupa hadhi ya jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote hapa ni mashahidi kwa namna ambavyo Mheshimiwa Rais amedhamiria na kuoneshwa kwa vitendo nia yake hii nzuri tutakumbuka alivyoanza mnamo tarehe 23 Julai, 2016 alipotamka na ninaomba kunukuu; "Leo tupo Dodoma kushiriki kwenye Mkutano Maalum wa CCM, napenda kutumia mkutano huu kueleza masuala mengine mawili ya ziada, jambo la kwanza hapa Dodoma ndio Makao Makuu ya Chama chetu pamoja na Serikali. Dodoma pia ni mji uliopo katika ya nchi yetu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limekuwa likifanya vikao vyake hapa, hata Chuo Kikuu kikubwa zaidi nchini kipo hapa Dodoma. Aidha, nimeamua maadhimisho ya sherehe za mashujaa mwaka huu yafanyike hapa Dodoma." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anaendelea; "hivyo kwa kutambua umuhimu wa Dodoma na pia katika kutekeleza ndoto za Baba wa Taifa letu Hayati Mwalimu Nyerere ya kuhamishia Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma, napenda kutamka mbele ya mkutano huu kuwa katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wangu nitahakikisha kuwa Serikali inahamia hapa Dodoma. Nitoe wito kwa Mawaziri na Watendaji wengine wa Serikali kujipanga kuhamia Dodoma hapa Dodoma kuna miundombinu ya kutosha hivyo naamini hapataatokea visingizio vya aina yoyote." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tamko hilo utekelezaji wake ukaanza mara moja na mpaka sasa viongozi wakuu wa Serikali akiwemo Makamo wa Rais, Waziri Mkuu na Wizara zote wamekwishahamia hapa Dodoma. Katika juhudi zake za kufanya Mkoa wa Dodoma kuendana na hadhi ya Makao Makuu ya nchi tarehe 26 Aprili, 2018 wakati wa sherehe za miaka 54 ya Muungano Mheshimiwa Rais alifanya jambo lingine kubwa kwa kutamka kuwa Mji wa Dodoma kuanzia tarehe hiyo sasa ni Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo limeleta hamasa kubwa kwa wananchi wa Dodoma na viongozi mbalimbali tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba bado tunasubiri mchakato wa kukamilisha suala la kuhamia Dodoma na urasimishaji wa Jiji la Dodoma kisheria, mimi binafsi, Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Dodoma, Waheshimiwa Wabunge wengine wote, Watanzania wote na wadau mbalimbali kwa ujumla tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake huo na kwa nia moja naleta azimio hili kumpongeza na kumuunga mkono kwa jitihada zake anazozifanya kumuenzi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere za kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la

kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uamuzi wake wa kuendelea Mji wa Dodoma na kuupa hadhi ya Jiji. Azimio hili nalitoa chini ya Kanuni ya 54 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA tangu aingie madarakani Rais wa Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli amefanya mambo makubwa ya kuendeleza Mkoa wa Dodoma; miongoni mwa mambo aliyoyafanya ni pamoja na uamuzi wake wa kuhamishia shughuli za Serikali kuja hapa Makao Makuu Dodoma; yeye mwenyewe kuonyesha dhamira ya kuhamia Dodoma pamoja na kuutangaza Mji wa Dodoma kuwa Jiji, tukio alilolifanya siku ya Sherehe za Muungano tarehe 26 Aprili, 2018;

NA KWA KUWA mambo haya makubwa anayoyafanya kwa Mkoa wa Dodoma yameleta hamasa kwa wananchi na mwamko mkubwa wa uendelezaji wa Mkoa wa Dodoma ikiwemo ongezo la Idara na Taasisi za Serikali kuhamia rasmi Dodoma na baadhi ya Mabalizi na Taasisi za Kimataifa kuonesha nia ya kujenga na kuhamia Dodoma; aidha, kutokana na hilo, wananchi wengi wamehamasika na kuanza kujenga nyumba bora za makazi, uwekezaji katika huduma mbalimbali za jamii umeongezeka; Serikali imeanza ujenzi wa miundombinu mbalimbali kwa mfano, kupanua uwanja wa ndege wa Dodoma, ujenzi wa barabara ya kuzunguka Jiji la Dodoma, ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Ihumwa na kadhalika;

NA KWA KUWA kitendo cha kuupa Mji wa Dodoma hadhi ya Jiji kitaleta manufaa makubwa, kwani hata mgawanyo wa rasilimali (*resource allocation*) utaongezeka ili kukidhi uendelezaji na uendeshaji wa huduma mbalimbali za kijamii zinazoendana na hadhi ya Jiji kama vile upatikanaji wa viwanja vilivyopimwa, majisafi na taka, huduma bora za afya na miundombinu imara ya barabara;

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

NA KWA KUWA pamoja na kwamba mchakato wa kisheria wa kurasilisha tamko la Mheshimiwa Rais unaendelea, maamuzi yake aliyoyafanya yamepokelewa kwa hamasa na shukurani kubwa na wananchi wa Dodoma kwa ujumla; Wawakilishi wa wananchi na viongozi mbalimbali wa Mkoa pamoja na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

HIVYO BASI Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Moja, Kikao cha Hamsini, tarehe 13 Juni, 2018 linaazimia kwa kauli moja kama ifuatavyo:-

Moja, kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na kumuunga mkono kwa uamuzi wake wa kuifanya Dodoma kuwa Jiji na hivyo kuliandaa Jiji la Dodoma kuendana na hadhi ya Makao Makuu ya Serikali. *(Makofi)*

Pili, kuiomba Serikali kuongeza rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali itakayoendana na hadhi ya Makao Makuu ya Jiji, kama vile ujenzi wa barabara zenye kiwango, miundombinu ya majisafi na majitaka, upimaji na upangaji mzuri wa Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Tatu, kuitaka Serikali ikamilishe haraka mchakato wa kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu na ikiwezekana Muswada huo usomwe kwa mara ya kwanza katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge unaoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, nakushukuru wewe kwa kukubali wazo hili na kutoa nafasi ya azimio hili liweze kuwasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Vigelegele)*

(Hoja lilitolewa lamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsanteni. Huku vipi? Upande huu hamtaki Dodoma iwe Mji?

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Hamna nguvu? Haya. Ahsante sana Mheshimiwa Simbachawene.

Sasa tunaanza kujadili, kwa upande wa CCM dakika tatu/tatu. Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Mariam Ditopile.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono azimio hii kwa asilimia mia moja. Mji wetu wa Dodoma umekuwa ni mji wa siku nyingi na Baba wa Taifa alipotamka kwamba Makao Makuu yahamie Dodoma tangu mwaka 1973 ni miaka mingi mpaka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais Magufuli kwa juhudi zake kuhakikisha kwamba sasa anatekeleza lile agizo au wazo la Mheshimiwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwamba sasa Dodoma iwe Makao Makuu. Dodoma ni Jiji kubwa, Dodoma makazi yake yamejengwa vizuri, hakuna *squatters*, tumefuata *master plan*, watu wameongezeka, kwa hiyo, kwa kweli kuna haja ya kupata Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyopata Jiji la Dodoma, hata sisi kwenye Wilaya zetu lazima kuna mambo mengi yataboreka kuhusu barabara, huduma za shule, huduma za maji na huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono azimio hili alilosema mdogo wangu Mheshimiwa Simbachawene kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bura na Mheshimiwa Mariam Ditopile ajiandae.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na nichukue nafasi hii kuunga mkono azimio ambalo lipo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tangu mwaka 1973 Mji huu wa Dodoma ulishapangwa kuwa Makao Makuu. Umechukua muda mrefu sana takribani maisha ya mtu mzima Serikali ya Tanzania kuhamia katika Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano kwa maamuzi haya ya haraka na mazito aliyoyachukua kuhakikisha kwamba Serikali sasa inahamia Dodoma. Naamini Marais waliomtangulia awamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne walifanya kazi kubwa ya maandalizi, naye amekuja kuhitimisha lile lililokuwa hamu ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ramani au *master plan* iliyojenga Abuja Nigeria, ilikuwa *master plan* ya Mji wa Dodoma. Ukienda Abuja, unaiona Dodoma ambavyo ingekuwa katika miaka hiyo. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwamba amewachukuwa wataalam wengi wa ardhi, amewapeleka maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba Mji wa Dodoma unakuwa tofauti na mikoa mingine kwa sababu ni Mji Mkuu uliosubiriwa kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza tena Mheshimiwa Rais kwamba ametoa fedha kwa ajili ujenzi wa *stand* ya mabasi ya kisasa ambayo litajengwa katika eneo la Nane Nane.

Pia tunajenga uwanja wa michezo wa kisasa ambao utajengwa hapa Dodoma na utachukua takribani watu zaidi ya 100,000. Pia tuna soko la kisasa ambalo halijawahi kujengwa Tanzania katika Mkoa wowote, ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi na ameomba msaada kutoka kwa watu wa Morocco kwa ajili ya ujenzi wa uwanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa Muswada wa Sheria uje kwa ajili ya kuutambua sasa Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali. Naiomba sasa Serikali ifanye haraka kuleta huo Muswada ili sasa Dodoma hata atakapokuja Rais mwingine asiyependa Mkoa wa Dodoma au Mji wa Dodoma, basi asipate nafasi ya kuhamisha Makao Makuu kupeleka Mkoa mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana hili azimio na ninaunga mkono azimio hili lililoko mbele yetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ditopile ajiandae Mheshimiwa Mtolea.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Awali ya yote napenda kusema kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Simbachawene kwa asilimia mia moja. Pia nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa kweli amekuwa kwa hakika akiwa ni mtekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kulifanya Dodoma kuwa Jiji, tuna uhakika sasa kweli Makao Makuu ya nchi yapo Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, narejea tena kumpongeza Mheshimiwa Rais na nimwambie, mimi kama mwakilishi wa vijana kutoka Mkoa wa Dodoma ambao sisi ndio tupo zaidi ya asilimia 60 ya *population* kwamba hilo tumelipokea na kwa kweli tutapokea changamoto zote na Dodoma kweli litakuwa Jiji. Niseme tu, kwa hili kumrudishia, tunajua mtanange 2020 upo, atashinda kwa asilimia kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna nchi za wenzetu hapa Afrika zimeweza. Mfano Nigeria na ya pili, *South Africa*. Kama wao wameweza na sisi tutaweza. Kwa hiyo, kama kuna mtu yeyote ambaye hajaunga mkono hoja hii, ajue kwamba sisi tumeweza na tutaweza. Kwa hiyo, la msingi tu apande pamoja na sisi tushirikiane kwa ajili ya kuhamisha Makao yetu Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mheshimiwa Rais alisema Morogoro kwamba katikati pazuri. Dodoma tumelala katikati ya nchi ya Tanzania na tunaona barabara imejengwa chini ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kuunganisha Iringa, Arusha na nchi ambazo zipo Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuweka Makao Makuu hapa katikati kutarahisisha hata uchumi wa ujenzi wa viwanda na huduma zote. Mtu kutoka Arusha ili apate huduma za Kiserikali hawezi kuzunguka kwenda mpaka Dar es Salaam. Mtu kutoka Iringa, Mbeya ni rahisi kufika Dodoma kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme jamani, katikati pazuri. Kweli Mheshimiwa Rais tunamshukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Abdallah Mtolea, dakika nne.

MHE. ABDALLAH S. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala hatubishani Dodoma kuwa Jiji au siyo Jiji, au Dodoma Kuwa Makao Makuu au siyo Makao Makuu. Tayari hapa ni Makao Makuu na tayari imetangzwa kuwa ni Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji kuwa Jiji *is not honorarium privilege*, ni vigezo, yaani Mji unakuwa Jiji kwa kuwa na vigezo. Mheshimiwa Simbachawene amekuwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI anafahamu Majiji yana sifa gani na Dodoma imepungukiwa sifa gani. Sasa kumuunga mkono Rais kwa hili alilolifanya ya kuifanya Dodoma iwe Jiji kabla haijawa na vigezo vya kuwa Jiji ni kutekeleza vigezo vile kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitegemea azimio linalokuja hapa liwe la Bunge kuitaka Serikali itenge

fedha za kutosha sasa ili twende tukaijenge Dodoma iwe na sifa ya Jiji. Tukisema tu tunapongeza kwamba tayari tumeambiwa na sisi ni Jiji, uneweza ukaitwa Jiji lakini bado ni kijiji. Hii haikusaidii! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma ambayo leo ni Jiji haina hata *stand* ya magari kutoka mkoani; Dodoma ambayo leo ni Jiji haina hata *stand* ya Daladala, zinasimama kokote tu, zinajipanga humo barabarani. Sasa tunahitaji fedha kuhakikisha Dodoma inapangika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu pekee ya *adventure* hapa Dodoma ni Mnadani. Mnadani ni kuchafu ajabu! Halmashauri inashindwa hata kutengeza basi. Sawa, tutakuja kuumwa kipindupindu hapa kwa sababu hatuna sehemu nyingine ya kwenda. *Weekend* lazima uende Mnadani. Unaenda kula, maeneo ni machafu. Halmashauri ibadilishe *mindset* zake kwamba sasa hivi hapa ni Jiji. Sasa Jiji lina heshima yake na Jiji ni vigezo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawataka Waheshimiwa Wabunge wa Dodoma watumie fursa waliokuwa nayo kuwa-*lobby* Waheshimiwa Wabunge hapa tuilazimishe Serikali kutenga fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hazipitiki huko, ikinyesha mvua ni tope kila sehemu. Fedha ya Halmashauri huwezi kujenga barabara zote hizo kwa kiwango cha lami. Barabara ya kilometa moja sasa hivi kwa lami ni kati ya shilingi milioni 900 mpaka shilingi bilioni 1.3. Halmashauri ya Dodoma mna fedha hiyo ya kujenga hizo barabara? Hamna! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya maji bado ni kile kile vya Mzakwe, watu wanaongeza, Mji unapanuka, hakiwezi kutosha. Leo mnagawa viwanja, Halmashauri iko *busy* kutangaza kugawa viwanja. Nendeni mkajenge miundombinu kule watu watakimbilia wenyewe. Unauza viwanja au mnauza mashamba sasa? Kwa sababu ili muuze viwanja na watu wavikimbilie ni lazima mtengeneze barabara, mpeleke umeme, pelekeni miundombinu ya maji,

watu watahamia. Leo hata ukijenga kule Mtumba utaenda kukaa? Huwezi kwenda kukaa, tutaendelea kubanana hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri Waheshimiwa Wabunge wa Dodoma mjipange vizuri ili tuweze kuwasaidia tuijenge hii Dodoma. Nasi tunakaa hapa, shughuli zetu tunazifanya hapa, tungependa pawe na hadhi ya Jiji na siyo hii blah blah tunayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yahaya Massare ajiandae Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niseme kwamba naunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Simbachawene kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangazo la Mheshimiwa Rais siku ile ya sherehe za Muungano kwamba sasa Dodoma limekuwa Jiji, limewafarijisha pia wananchi wa mkoa ya jirani ukiwepo Mkoa wa Singida kwamba Jiji litakapokuwepo Dodoma nao watapata fursa mbalimbali zikiwemo za kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutangaza, lakini kabla hajatangaza, alifanya kazi moja kubwa ambayo ilikuwa ni kero iliyopelekea wananchi wa Dodoma kuwa na mtafaruku, mamlaka mbili zilikuwa zinausimamia Mji huu; Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma lakini wakati huo huo kulikuwa na Mamlaka ya CDA. Kwa kuivunja Mamlaka ile ya CDA kumetoa fursa sasa kwa Jiji la Dodoma kusimamiwa na mamlaka moja ambayo itaupanga Mji, lakini kuhakikisha inafanya maendeleo kwa ajili ya wananchi wa Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii lakini nikiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano isaidie Jiji la

Dodoma kuhakikisha kama ilivyofanya Jiji la Dar es Salaam, kitengo cha Wizara ya Ardhi kiondoke katika Jiji kiende Wizara ya Ardhi ili kuondoa mtafaruku ambao utakuja kupelelekea *squatters* tena zianze kuwepo Dodoma. Viwanja vipimwe vya kutosha, miuondombinu ipelekwe, lakini wakati huo huo Halmashauri ya Jiji ishughulikie na ukusanyaji na mapato yake ili kuboresha Jiji ili tuweze kufanya Jiji hili liwe la mfano lakini Jiji la kielelezo kama yalivyo Majiji mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majiji yetu mengi katika nchi hii yamepangwa vibaya. Jiji hili la Dodoma ikiwa Manispaa, lilikuwa limepangwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa naiomba Serikali ije na mchakato katika Bunge hili kuleta sheria ya kutangaza sasa Jiji hili la Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, ajjandae Mheshimiwa Mwambe.

MHE. ZUBEIR M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja hii iliyoko mbele yetu. Awali ya yote niseme kwamba siungi mkono hoja hii kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sijaelewa kipi kitatangulia? Hivi ni vigezo vinatangulia kuwa Jiji au Jiji ndiyo linatangulia halafu vigezo vifuate? Kwa sababu ukiangalia azimio hili, aya ya pili ya Mheshimiwa mtoa hoja anasema, anaiomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya miuondombinu ya kuboresha Dodoma. Sasa sijaelewa kwamba ina maana yeye anakubali kwamba bado hatujafikia vigezo vya Dodoma kuwa Jiji. Kwa hiyo, anaiomba Serikali sasa itenge fedha ili Dodoma iwe Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeeunga mkono hili azimio kama Mheshimiwa Rais angetamka kwamba nataka kufikia

mwaka 2020 – 2025 Dodoma iwe Jiji. Ndiyo maana nasema sasa Serikali ijipange kwamba Dodoma iwe Jiji. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu ninavyofahamu, Dodoma kuwa Jiji tayari ni mradi. Tayari inatakiwa bajeti itengwe kwa ajili ya Dodoma kuwa jiji. Hii ndiyo sababu leo hii hata kuhamia Dodoma. Tulihamia hivi hivi, kuhamia Dodoma ni mradi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako lilitenga bajeti ya kuhamia Dodoma? Leo hii Bunge limetenga bajeti kwa ajili ya Dodoma kuwa Jiji? Sasa mambo yote haya, hakuna mtu anayepinga Dodoma kuwa Jiji, lakini Mheshimiwa Rais angetamka kwamba nataka kufikia mwaka 2020 au 2022 nataka Dodoma iwe Jiji halafu miundombinu ifuate, kama ambavyo mtangulizi wangu alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Dodoma hatuna *stand*, leo hii uwanja wa ndege uko mjini pale, wala haufai. Tunahamishia wapi? Tunahamishia Msalato; *stand* ya bodaboda na kadhalika tunahamishia Nanenane. Maana yake ni kwamba tunataka tutengeneze miundombinu ili Dodoma iwe Jiji...

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Kuchauka kwamba hata Jiji la Dar es Salaam, miundombinu siyo kwamba imekamilika. Bado kuna miundombinu ambayo inaendelea ikiwemo na *flyover*, lakini lile *still* ni Jiji.

Kwa hiyo, suala la miundombinu ni suala endelevu hata katika miji mikubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, endelea.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na taarifa yake siipokei. Nilichokiongea ni kwamba vigezo vitangulie kabla ya kutangazwa kuwa Jiji. Dar es Salaam anayoisema ni kwamba ilitangulia vigezo vya kuwa Jiji. Ile inayoendelea sasa hivi pale ni nyongeza tu. Hatuna maana kwamba Dodoma itakapojengwa kuwa Jiji, hiyo miundombinu ikikamilika haitaendelea tena kujengwa. Maana yake ni kwamba miundombinu itakuwa inaboreshwa kila wakati. Ninachokisema na ndiyo maana *CDA* ilivunjwa, kwa sababu haikutimiza malengo yaliyokuwa yamekusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu ya Kwanza tangu mwaka 1973 alitangaza kwamba Makao Makuu ya nchi hii iwe Dodoma, lakini akaunda na mamlaka ile ya *CDA*. Kwa sababu *CDA* hawakufikia vigezo na ndiyo maana Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano akaja akaivunja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda niseme kwamba Bunge lako tukufu ili liweze kuunga mkono hoja hii, basi kauli hiyo ibadilishwe kwamba Mheshimiwa Rais ametamka kwamba kufikia mwaka fulani, Dodoma inatakiwa iwe Jiji. Leo hii Dodoma bado haijakidhi vigezo kuitwa jiji. Kama tukiamua kuweka jiji kisiasa, twende tuliweke jiji kisiasa, lakini vigezo bado havijakamilika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia. Kama ambavyo wengine wamesema kwamba nia hii inaweza kuwa njema kabisa, lakini njia za kwenda kufikia kwenye utekelezaji wa hii nia ndiyo ambazo watu wanajaribu kuzisema ili tuweze kurekebisha. Ukienda kwenye Majiji, kati ya vigezo ambavyo vinatakiwa ni pamoja na kuwa na idadi ya watu fulani. Kwa mfano, lazima uwe na watu

wasiopungua 500,000 ili uweze kutengeneza jiji kama kigezo. Ukija Jiji la Dodoma hili ambalo sasa hivi tunaenda kuliita jiji ni kati ya Majiji ambayo yanaanza kuongoza kwa vituko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais kwa mara ya kwanza ndio amemchagua Meya wa Jiji la Dodoma, kitu ambacho hata kisheria hakipo. Kwa utaratibu, Meya huwa anachaguliwa na Madiwani wenzie kutokana na Baraza la Madiwani, lakini hapa tumeona. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangaia hata *presenter* wakati mwenyewe Mheshimiwa anaongea pale, *he was not happy*, yaani hafurahii kile anachokifanya, ni kama amesukumwa au kuna watu wanamlazimisha kukifanya au kuna kitu wanakitafuta ili kuweza kuwafurahisha watu fulani wakati kimsingi vigezo havijatimia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemsikiliza vizuri hapa Mheshimiwa Mtulia hapa wakati anachangia, wote tungeelekea kwenye mwelekeo ule wa Mheshimiwa Mtulia ili kuweza kupata Jiji bora la kihistoria na la mfano. Viongozi wanafanya jambo la maana, lakini tunakuja hapa ni kupongezana na kusifiana kwenye vitu ambavyo havijafanywa vizuri. Hili siyo jambo jema sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti ulifanyika, wakasema ili kufanya Dodoma iwe mji au Makao Makuu ya nchi kunatakiwa *40 trillion* ili kuliboresha hili jiji na wakashauri kwamba hii *transition* ifanyike kwa muda wa miaka kumi angalau wafikie milioni nne kutokana na udogo na huu ufinyu wa bajeti yetu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Sasa ukiangalia sasa hivi hata hawa watumishi...

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa rafiki yangu Mwambe kwamba Meya wa Jiji la Dodoma kwamba alichaguliwa na Rais na anapaswa kuchaguliwa na Madiwani, labda amekosea. Meya ambaye ni Profesa Mwamfupe, ni Diwani ambaye alichaguliwa na Madiwani wenzake katika Manispaa ya Dodoma akawa Meya. Kwa hiyo, asije akachanganya Meya pengine na Wakurugenzi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona nimpe taarifa asije akapotosha wananchi kwamba Mheshimiwa Rais ndiye alimchagua...

MHE. HALIMA J. MDEE: Taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: *Order! Order! Order!* Anayezungumza ni mtu mmoja tu, wengine wote kaeni chini.

MHE. HALIMA H. MDEE: Atulie, aache kudanganya basi. Tutatoa taarifa sisi!

MWENYEKITI: Hebu Mheshimiwa Mwambe kaa chini. Umemaliza?

NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Akae chini huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo...

MWENYEKITI: Aaah! Waheshimiwa!

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nampa taarifa asije akapotosha umma pamoja na Wabunge kwamba...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Susan Lyimo, tulieni! Mheshimiwa malizia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namalizia kwamba Mheshimiwa Mwambe asiwapotoshe Watanzania. Meya, Profesa Mwamfupe hakuchaguliwa na Rais.... Alikuwepo kama Meya.

MWENYEKITI: Ahsante, nimeshakuelewa, fedha zipo. Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo unaona hali iliyoko hapa, hata huyo Meya mwenyewe uteuzi wake ulipitia kwa Mheshimiwa Simbachawene wakati huo ni Waziri wa TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona ile namna ya kutaka kubebana bado inaendelea wakati utaratibu haujaandaliwa. Anatakiwa kuwa Meya ambaye anatokana na uteuzi kwenye kata. Diwani wa Kata na sio mtu wa kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona watu wanaoteuliwa, usumbufu wanaotuletea, hata humu ndani ya Bunge, wanaoteuliwa wengi ndiyo ambao wanatuyumbisha kwa sababu wanafanya mambo tofauti na mahitaji ya watu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii nia inaweza kuwa njema lakini njia tunayotaka kutumia kwenda kutekeleza hii nia siyo nzuri. Tulete hiyo sheria ibadilishwe, zifuatwe taratibu zote za kutangazwa kwa Jiji, vinginevyo kule kote ambako wana nia ya kuwa na Majiji na Serikali hii ndiyo ambayo ilisema tunashindwa kuongoza, tunashindwa kupanua maeneo ya kijiografia kwa sababu ya kubana matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuangalie namna ambavyo sisi tunataka kwenda huko mbele, badala yake sasa yote haya yanayotokea ya kuteuliwa tutalazimisha jambo; sasa hivi ukija kuangalia hapa, hata omba omba wanashindwa kutoka Dar es Salaam kurudi Dodoma kwa sababu hapa hapajakaa vizuri bado kwa ajili ya zile kazi zao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiangalia upande wa pili, Watumishi wa Umma wanatakiwa wahamie hapa, lakini huko kuna migogoro. Pamoja na kwamba wake zetu, wengine waume zao ni watumishi wanatakiwa waje kujiunga nao Dodoma, lakini Dodoma bado hapajakaa kuweza kutangazwa kuwa jiji angalau tu kwa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna uhaba wa shule, kuna uhaba wa miundombinu, maji, umeme, vinakatika. Juzi tumetoka kulalamika hapa masuala ya umeme, tunaambiwa transfoma zilizopo haziwezi kuhudumia Dodoma kama Jiji. Haya leo tunataka watumishi wote wa umma wahamie hapa; wale wote wakijazana hapa vyoo vyetu vitaziba. Hali iliyoko Dar es Salaam itakuja kujitokeza na hapa tena. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, kimsingi lazima kwanza tuboreshe, tuhakikishe hapa hakuna haja ya kukimbilia hivi vitu, sisi tunakubali watumie muda mrefu kufanya Dodoma liwe Jiji, ibaki kuwa Makao Makuu ya nchi ili tuweze...

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) : Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kakunda kaa chini.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naombe Serikali irudi tena, Mheshimiwa Simbachawene arudi akatafakari, atafute ule utafiti uliofanyika aipelekee Serikali kwamba jamani hebu boresheni kabla hatujaamua kukurupuka na kwenda kutekeleza hili jambo kabla ya wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kujidhallisha tukianza kujilinganisha na Nigeria, mara sijui Somalia na kwingine kote. Tuangalie kwanza mahitaji ya wakati kabla ya hivyo vitu havijaja mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Hata mbuyu ulianza kama mchicha. Mheshimiwa Kubenea. *(Makofi/Kicheko)*

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwamba umenipa nafasi ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Simbachawene tuko Kamati moja ya Katiba na Sheria na anajua jinsi gani Serikali ilivyoshindwa kupeleka fedha za maendeleo katika Wizara nyingine na Ofisi ya Makamu wa Rais iliyolazimishwa kuhamia Dodoma ilivyopewa fedha nyingi sana kinyume/zaidi ya bajeti iliyoomba. Ni kwa sababu mipango ya kuhamia Dodoma, mipango ya kuufanya uwe Mji Mkuu haikuandaliwa. Tumekurupuka bila kuwa na vigezo, tumekurupuka bila kuwa na takwimu na tunafanya mambo haya kama vile nchi hii inakufa kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la kuufanya Dodoma kuwa Mji Mkuu ambayo ndiyo hoja ya Mheshimiwa

Simbachawene. Mji Mkuu umetangazwa kabla ya sheria kuja Bungeni. Jiji limetangazwa bila sheria kuja Bungeni. Sasa tunatangaza jiji halafu ndiyo tunaleta sheria, halafu tunapongezana hapa. Tunatangaza Makao Makuu ya nchi Dodoma wakati Jiji la Dodoma halijawa na sheria ya kuifanya Dodoma kuwa Jiji. Maana yake ni kwamba kumbe Mheshimiwa Rais alikuwa anakuja kuhamia kijijini, haji kuhamia kwenye Jiji. Hakuna sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo ni zuri na hakuna anayelipinga, lakini ni lazima tufuate taratibu. Kuna mikoa nchi hii imetimiza vigezo vyote vya kuwa jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi imetimiza vigezo vyote vya kuwa jiji, lakini Mheshimiwa Rais amekataa Moshi kuwa jiji na Mheshimiwa Simbachawene unajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine kwa sababu amesema watu wa Kaskazini wasimame kwanza, maendeleo yaende mikoa mingine, yawezekana amekataa Moshi kwa sababu watu wa Kaskazini wasimame kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MBUNGE FULANI: Kaa chini!

MWENYEKITI: Taarifa.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mzungumzaji. Pale anaposema kwamba Mheshimiwa Rais amekataa Moshi isiwe Jiji, analipotosha Bunge.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika, Mheshimiwa Rais alipokwenda pale, walisimama wadau wa Moshi wakasema hatujashirikiswa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais akaagiza mchakato uweze kurudiwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea endelea.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kwamba mtu aliyesimama wala hajui historia.

MBUNGE FULANI: Kabisa.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wakubwa wa Moshi ni Baraza la Madiwani, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kupitia Baraza la Madiwani na Meya wao Japhary Michael ambaye leo ni Mbunge wa Moshi Mjini walipitisha Azimio la Moshi kuwa Jiji. Vikao vya RCC vyote viliamua Moshi iwe Jiji. Anazungumza nini? Nimemsamehe kwa sababu hajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi ya kukurupuka, tunapozungumza hivi leo tunataka Dodoma iwe Jiji, tumeomba msaada wa kujenga uwanja wa mpira kutoka Morocco ili kuifanya Dodoma iwe na hadhi ya Jiji. Madhara yake ni nini? Madhara yake ni kwamba Morocco msimamo wa CCM hawa na Serikali hii kwa miaka yote tokea Baba wa Taifa tunatambua Sahara Magharibi. Leo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa nenda kwenye hoja iliyokuwa mezani.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hii.

MWENYEKITI: Nenda kwenye hoja ambayo iko mezani.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea...

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma hii watumishi wa umma wameletwa Dodoma. Ndoa zimevunjika, waume wako Dar es Salaam, wake wako Dodoma; wake wako Dar es Salaam, waume wako Dodoma, ndoa zimevunjika. Watu wameshindwa kuhama na wake zao na familia zao, mtu amebakisha miaka minne, leo analazimishwa aje Dodoma kabla ya kustaafu, imekuwa ni shida.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mdogo sana. Mheshimiwa kaa chini.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo amesimama au amekaa?

MWENYEKITI: Endelea, dakika yako imebaki moja tu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. SAED A. KUBENEA: Akae basi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina kaa. Mheshimiwa Kubenea endelea.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Dodoma ambayo imetangazwa Mji, Dodoma ambayo imetangazwa Makao Makuu ya nchi haiwezi kuunganisha na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Leo kutoka Rwanda, Waziri akitaka kufanya miadi ya Waziri Mkuu hapa Dodoma akitokea Rwanda hawezi kufika kwa haraka kulliko akifika Dar es Salaam. Hakuna *connection* kati ya Mkoa wa Dodoma na Mikoa mingine kwa usafiri wa haraka wa anga. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Ndiyo!

MHE. SAED A. KUBENEA: Sasa mnataka Dodoma iwe Mji, Dodoma iwe Makao Makuu, hakuna *international schools* hapa za kusoma watoto wa Mabalazi. Dodoma haijawa tayari na ninyi mnajua kwamba wapo watu waliofanya *research* wakasema baada ya miaka 10 ijayo kwa kutenga shilingi triloni nne kwa kila mwaka kwa muda wa miaka 10...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kubenea muda wako umekwisha. Muda wako umekwisha.

Kuhusu miundombinu, Bunge la Afrika Mashariki limekaa Dodoma, Wabunge wametoka maeneo yote wamekuja Dodoma, uwanja wa ndege wa Dodoma unachukua mpaka Boeing 757, uwanja unatumika usiku na mchana, uwanja umesadifika katika masuala ya usalama wa anga. Kaa chini. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Antony Komu, ajiandae Mheshimiwa Deo Sanga.

MHE. SAED A. KUBENEA: Nakushukuru.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia azimio hili na nianze kwa kueleza masikitiko yangu kuhusiana na azimio hili kwa sababu kwa maoni yangu ni azimio ambalo kwa kweli ni lenye ubaguzi kwenye nyanja nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema ni azimio lenye ubaguzi kwa sababu kwanza ukiangalia hili azimio, linataka kufanya historia kama inanza leo kwamba Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ndio ambaye amefanya hili Jiji la Dodoma au huu Mji wa Dodoma kuwa ndiyo Makao Makuu na kuwezekana kuwa Jiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kuifanya Dodoma ikawa kama ilivyo leo na Mheshimiwa Simbachawene amerejea hapa kwamba wakati Mheshimiwa Rais anazungumza kwenye Mkutano wenu Mkuu, alizungumza kwamba vipovitu ambavyo vimeshawezesha sasa Dodoma kuwa ni mahali panaweza kuwa Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo azimio hili lingekuwa na maana sana na ningeliunga mkono kama lingetambua vilevile watu wengine ambao wamefanya mambo makubwa mpaka tukawa jinsi tulivyo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu wamejenga hili Bunge, wako watu waliojenga barabara za kuja Dodoma, wako watu waliojenga Chuo Kikuu cha Dodoma. Hivi leo Rais Dkt. Magufuli amefanya nini ambacho ni muujiza? *(Makofi/Kicheko)*

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais, Mheshimiwa Magufuli ametangaza, tena ametangaza bila kuzingatia sheria. Amepoka mamlaka ambayo sio yake.

MBUNGE FULANI: Ya kwake.

MHE. ANTONY C. KOMU: Siyo, nenda karejee Sheria ya Mipango Miji kifungu cha 7(2) uone nani mwenye mamlaka ya kutangaza Mji kuwa Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunataka kuonesha Bunge hili kufanya kwamba fedha anazotumia Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni za kwake za mfukoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili ni lazima lijirudishe mahali pake liwe na hadhi na kwamba ndilo linaloombwa pesa. Serikali inapaswa kuja hapa kuomba pesa na siyo sisi Wabunge kuwa ni chombo cha kushangilia na kupongeza wajibu wa mtu anaopaswa kufanya. Hilo ndilo sikitiko langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikitiko la pili ni aina ya ubaguzi unofanywa katika kutekeleza mambo mbalimbali katika nchi. Sisi Moshi tulifanya michakato yote ya kuwa jiji kwa zaidi ya miaka mitano na tumetumia fedha nyingi za ndani na za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba Mheshimiwa Rais siku moja kabla ya Mei Mosi ya mwaka 2017 alikuja akakaa mahali na watu ambao sisi watu wa Moshi hatuwajui, akaamua kufuta mchakato mzima wa Moshi kuwa Jiji. Sasa hili sijambo la kushangilia. Ni jambo la kusikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mpango huu ni mpango wa kukurupuka. Ni mpango ambao unasababisha mateso makubwa kwa Watanzania. Leo...

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina, kaa chini.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, leo watumishi wa nchi hii...

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Amina nimekwambia kaa chini! (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze kwa masikitiko makubwa kwamba mwezi uliopita tumepoteza watumishi watatu wa *TIC* wakiwa wanakuja Dodoma wakisafiri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge na kwa Mheshimiwa Komu, kwa umri uliokuwa nao, mwaka 1973 najua tayari ulikuwa na upeo mkubwa sana. Mwaka 1973 wakati nchi ipo katika ukombozi wa Bara la Afrika, Afrika Kusini ilituma ndege Kusini mwa nchi yetu Mtwara.

Waheshimiwa Wabunge, ile ndege ikapata bahati ikaangushwa na vyombo vyetu. Ndege nyingine zikawa zinatumwa Mkoani Dar es Salaam kuja kumwaga vipeperushi vya uongo, Mwalimu na vyombo vyake vya ulinzi wakaamua lazima makao ya nchi yakae Dodoma kwa sababu ya usalama. Nilitaka nikueleze tu ulifahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa mtoa hoja. Mheshimiwa Deo Sanga, nilikuita subiri. Mheshimiwa Munde.

MBUNGE FULANI: Alikuwa hajajiandaa.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unaita watu gani? Watu walioomba mbona huwaiti?

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wote waliompongeza Mheshimiwa Rais kwa wazo hili, lakini naungana na Waheshimiwa Wabunge wote waliompongeza Mheshimiwa Rais kwa maamuzi magumu aliyoyafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke Rais huyu ana muda wa miaka miwili na nusu au mitatu, hajatimiza mitatu kamili, lakini amefanya mambo makubwa sana ikiwepo kuamua maamuzi magumu ya kufanya Mji wa Dodoma uwe Makao Makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi mwanzo nilipata *shock* alivyoamua kipindi kile mwanzo tu anaanza. Kwa sababu wakati anaamua ndiyo alikuwa ameamua elimu bure, ndiyo alikuwa ameamua kujenga reli, kununua ndege, kujenga *flyover*, ndiyo alikuwa mambo chungu mzima katika nchi hii. Nikasema jamani yatawezekana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mshangao mkubwa, leo hii Mji Mkuu wa Dodoma...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Kaa chini.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: ...na unaendelea kwa kasi kubwa sana, mambo yote mengine ya reli yanaendelea, ndege zimeendelea kuja na karibu zitafika saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono hoja hii aliyoitoa Mheshimiwa Simbachawene.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naitakia Serikali yangu kila la heri pamoja na Mheshimiwa Rais ili waweze kutimiza jambo hili na wale wote waliyokuwa wanaona kwamba haiwezekani, basi waje waone aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti juzi tu wametokeleza kugawa *tablets* kwa shule zote za msingi jambo ambalo huwezi kuliadini kwa haraka haraka ukizingatia Rais huyu ana muda wa miaka miwili na nusu tu. Amegawa *tablets* ili walimu wetu wa shule za msingi wazidi kufundisa vizuri. Angalau Mheshimiwa kaka yangu Sugu alisema ile ni ahadi hewa, lakini nimpe taarifa tu kwamba Mheshimiwa Rais ameshaitekeleza, sasa hivi walimu wa shule za msingi wanatumia *tablets*. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, naendelea kumwombea kila la heri ili aweze kufanya yale yote aliyokuwa ameyakusudia na tutaendelea kumuunga mkono na kumtia moyo pale panapostahili. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. (Makofi/Vigelegele)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakyembe halafu wajiandae Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga kwa kweli ni kuchagua na uteuzi wa Makao Makuu ya Nchi unaendana na matakwa ya wenye nchi wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kwamba naunga mkono Azimio hili na niwakumbushe tu ndugu zangu historia fupi kwa kifupi tu kwamba mwaka 1891 Mjerumani alipoitwaa nchi yetu kuitawala wakati huo ikiitwa *Deutsch-Ostafrika* ikiwepo na Rwanda na Burundi, akateua Kijiji cha Bagamoyo kuwa Makao Makuu ya *Deutsch-Ostafrika*. Wakati huo Bagamoyo ilikuwa na nyumba moja tu ya bati, lakini uteuzi huo ulikuwa na maana ya kuweka changamoto kwamba sasa inajengwa Bagamoyo kuwa sasa ndiyo *capital* na Jiji la *Deutsch-Ostafrika*. Baadae ikahamia Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana naomba tu nipongeze uamuzi tu wa kuhamia Dodoma na uamuzi wa

kutangaza Dodoma kuwa Jiji, kwamba hii inakamilisha uhuru wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi wa Dar es Salaam na Dodoma ulikwenda na vigezo vya mkoloni kwamba alihitaji sehemu ambayo atanyonya chochote kilichoko Tanganyika na kukipeleka kwao. Sasa tunajiangalia ndani, tunahitaji Mji Mkuu ambao uko katikati ya Tanzania, ambao utatuhudumia wote kwa pamoja. Ndiyo maana tunaunga mkono uamuzi huu wa kijasiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimweleze tu kidogo ndugu yangu Mheshimiwa Kubenea anasema kwamba usafiri kuja Dodoma ni mgumu sana. Ni kawaida miji yote ambayo imekuwa mikuu baadae, leo usafiri kwenda Lagos ni rahisi kuliko kwenda Abuja. Safiri kidogo Mheshimiwa Kubenea, usikae tu kwenda Bagamoyo. Vilevile nenda Uganda, usafiri kuingia Entebe ni rahisi kuliko kwenda Kampala. Ni vitu vya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda haujaniishia, nimalizie tu kusema tu, ndugu zangu hebu tumwache Mheshimiwa Rais atekeleze majukumu yake kwa kufuata Katiba hii. Hebu niwasomee tu Ibara ndogo ya 37 ndiyo niishie hapa, inasema; "Mbali na kuzingatia masharti yaliyomo katika Katiba hii na Sheria za Jamhuri ya Muungano katika utendaji wa kazi na shughuli zake, Rais atakuwa huru na hatalazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote." *(Makofi/Vigelegele)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jafo. Mheshimiwa Zitto kaa, tafadhali.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuunga mkono hoja iliyotolewa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu, katika watu

wanatuishi kwa upendo mkubwa sana sisi Waheshimiwa Wabunge ni ndugu zetu wa Dodoma. Kauli zetu zisiwafadhaishe wenyeji wa Dodoma. Hili ni jambo la kwanza, lazima tuliweke sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wWakati Mheshimiwa Rais anakusudia hili jambo jema ambalo lina maslahi mapana kwa nchi yetu, halafu na sisi viongozi tuliopeva dhamana tukionekana tunatoa mishipa kama vile jambo hili siyo jema, nadhani tunawanyong'onyeza sana kwa kiwango kikubwa wenyeji wetu wa Dodoma, hili ni moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kwa sababu Azimio hili lilikuwa ni suala zima la maelekezo ya kisheria ije Dodoma. Niseme kwamba Ofisi yangu ipo katika maandalizi ya mwisho kabisa ya hii sheria ya kuja Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika suala la miundombinu, Ofisi yangu ambayo ina mamlaka ya kufanya hivyo, mwaka huu hapa Dodoma tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 35 kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa, *stand* ya kisasa pamoja na *recreation area*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kupitia *TARURA* lengo letu ni kwamba tunataka tutengeneze barabara za pete za kutosha, nanyi sasa mnafahamu, hata ukitoka *St. Gasper* unakuta barabara nyingine zimefunguka. Lengo letu ni kwamba tuwe na *ring road* za kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie ndugu zangu, Dodoma ndiyo itakuwa ndiyo Mji wa kwanza *the best* hapa Tanzania kwa upangaji mzuri. Ofisi yangu imeelekeza na hivi sasa tumekamilisha viwanja 15,000 eneo la Mtumba vimekamilika na hivi sasa watu wapo foleni kugombania hivyo viwanja kwa ajili ya mustakabali wa Dodoma. Kuna viwanja 21,000 tunavipima maeneo ya Ihumwa kule. Lengo letu ni kwamba tuhakikishe Mji wa Dodoma ndiyo Mji mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu, hata ukiwa unashuka na ndege, ukiwa

unashuka Dodoma ni tofauti kama unaposhuka maeneo ya miji mingine. Hili ni jambo la kujivunia kwetu sote. Kubwa zaidi katika hili, najua Mheshimiwa Rais amepewa kwa mujibu wa Sheria Sura Na. 288 katika kifungu cha (5)(3) katika suala zima la uanzishaji miji, tukipitia sheria tutajua haya mambo ni jinsi gani Mheshimiwa Rais hakukurupuka alifanya kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika kwa sababu Mheshimiwa Rais amepewa dhamana na Watanzania na dhamana aliyopewa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani imeainisha jinsi gani Serikali hii itahamia Dodoma. *(Makofi)*

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Ulitaka kuongeza kidogo. Ongeza nusu sekunde nakupa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika agenda ya *comparison*, nadhani kuna kitu kidogo kilikuwa na sintofahamu kuona kwamba Mheshimiwa Rais kwa nini aliwabagua watu wa Moshi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie ndugu zangu, Moshi kilomita za mraba ni 58 peke yake. Naomba niwaambie, tukienda katika utaratibu wa vigezo, Wabunge wa kule wanafahamu. Ndiyo maana kulikuwa na suala zima la *extension* hata kuhakikisha kwamba kuna vikao vingine watu Hai watenge maeneo yao kwa ajili ya jiji la Moshi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mambo haya yalikuwa katika mchakato zaidi. Kama Moshi yenyewe, kilomita za mraba pale ni 58, naomba tuelezane ukweli. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja kwanza, nawaeleza *fact*, kwa nini kila jambo linaenda kwa mujibu wa sheria? Ukianza hilo sasa, ndiyo maana hata Moshi yenyewe naomba niwaambie, wewe Mheshimiwa Komu, subiri... (*Makofi*)

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komu kaa chini. Mheshimiwa Jafo malizia.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais jambo lolote anashauriwa kwa wema. Naomba niwaambie, hakuna jambo lolote unaweza ukashauri kwa hasira. Kila kitu busara inatawala kufanya mambo yaweze kukamilika. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kabla sijaendelea, nachukua nafasi hii kuunga mkono Azimio lililoletwa na Mheshimiwa George Simbachawene. Ninaunga mkono Azimio hilo na niseme tu kwamba ukweli ni kwamba jambo hili wala siyo jambo la kukurupuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 151 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi iliielekeza Serikali ndani ya miaka mitano ihakikishe kwamba Serikali imehamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Ibara hiyo ya 151 iliweka bayana mambo ambayo hata azimio hili limeyaelekeza. Ilani ilisema la kwanza; Serikali ihakikishe kwamba majengo yote ya Serikali yaanze kujengwa Dodoma kitu ambacho tumeanza kukifanya. Ilani imeelekeza, viwanja vipimwe katika Mji wa Dodoma Makao Makuu kwa ajili ya shughuli za Serikali na wananchi wa

Tanzania. Mheshimiwa Jafo, amesema na ndivyo tunavyofanya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ilani imeelekeza itungwe sheria ya kutambua Dodoma kuwa Makao Makuu, ndiyo azimio ambalo linaletwa leo. Kwa hiyo, tuna kila haja ya kuunga mkono Azimio hili lililoletwa na Mheshimiwa George Simbachawene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme yafuatayo: sisi kama Serikali tunampongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Serikali zote zilizotangulia nakubaliana sana na Mheshimiwa Komu zilitengeneza mazingira wezeshi, lakini maamuzi ya kuhamia Dodoma kulifanya Dodoma kuwa Jiji, kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu yamefanywa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na anastahili kupewa pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema tunapohamia hapa Dodoma sasa, tumeweza kutekeleza, tumetekeleza kwa vitendo na tunapotekeleza kwa vitendo na kumuenzi Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, maneno haya aliyatamka Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na sisi tumeyatekeleza mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niliarifu Bunge hili, mnaposema kwamba kuna mgongano wa wafanyakazi kuhamia hapa Dodoma, ninaomba niwaambie kati ya wafanyakazi 7,440 wa Wizara zote wanaotakiwa kuhamia hapa Dodoma tumebakiza wafanyakazi 909 tu, wengine wote wameshamia hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wafanyakazi hawa kuhamia hapa Dodoma, Waheshimiwa Wabunge wanafikiri kutakuwa na migongano ya miundombinu, lakini mpaka sasa mmeona Dodoma ni shwari na shughuli za Serikali zinatekelezwa kama inavyotakiwa na hakuna tatizo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuthibitishie, kama Serikali tutaendelea kulisimamia agizo hili la Mheshimiwa Rais, kutekeleza matakwa ya Marehemu Baba wa Taifa na azma ya Ilani ya Uchaguzi Ibara ya 151. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona adui yako anakusifia, ujue umeharibu, lakini ukiona adui hasifii unachokifanya, ujue umefanikiwa. Kwa hiyo, sisi tutaendelea kuifanyia kazi azma hii njema ya kuhamia hapa Dodoma. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mtoa hoja, dakika tano. Mtoa hoja dakika tano. Toa hoja usiwasilize watakupotezea muda.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia. Nawashukuruni sana. Waheshimiwa Wabunge wote kwa pande zote mbili kimsingi ni kama wameunga mkono hoja yangu na hoja ya Wabunge wa Mkoa wa Dodoma ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuamua Dodoma kuwa jiji. Kimsingi ni kama wamepongeza na wameunga mkono hoja hii nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tulileta hoja hii? Tulileta hoja hii ya kuomba azimio hili lipitishwe na Bunge kwa sababu ni utaratibu wa kawaida wa mabunge duniani. Pale ambapo Serikali imefanya jambo zuri, ni jambo zuri la kidiplomasia pia kuungwa mkono na Bunge lake ili kuonesha kwamba Bunge na Serikali viko pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi ulifanywa mwaka 1973, ni miaka 44 mpaka 2017. Rais huyu wa Awamu ya Tano baada ya kupita Marais wengi, yeye ameamua kwa vitendo kwamba tunahamia Dodoma, Serikali inahamia Dodoma mambo ambayo tayari yameshafanyika. Kwa hiyo, tunapotaka kupongeza ni kwa sababu sisi Wabunge wa Dodoma

tunaona faida inayopatikana na ninyi wenzetu Wabunge mnaona yanayoendelea kwamba Dodoma inashamiri na inaenda kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapooona matembe yaliyokuwa karibu na mji yanaondoka, tunapooona watu wanazidi kujenga nyumba bora, tunapooona miundombinu mbalimbali inazidi kuimarishwa, tunapooona idadi ya watu inaongezeka, tunapooona Wabunge badala ya *weekend* kuondoka kwenda Dar es Salaam mnabaki Dodoma, sisi mlitaka tufanye nini badala ya kuomba tupitishie Azimio hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tumeomba Azimio hili lipitishwe na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wote tunge mkono, kwa sababu Rais huyu amefanya jambo kubwa na sisi Wabunge wa Dodoma tunataka Watanzania wafahamu kwamba Wabunge wa Dodoma tumefurahishwa na jambo hili na tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Afrika ijue kwamba Wabunge wa Dodoma na wananchi wa Dodoma tumefurahishwa na jambo hili, tunataka dunia ijue kwamba Wabunge wa Dodoma na Watanzania kwa ujumla tumefurahishwa na jambo hili na ndiyo maana tunaleta azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es Salaam ilipotangazwa kuwa jiji ilikuwa haijakidhi vigezo na ile siku ya Uhuru ikatangazwa Dar es Salaam kuwa Jiji. Ilikuwa haina hata vigezo hata kimoja. Tuna Jiji la Mbeya, Jiji la Tanga, Jiji la Arusha na Jiji la Mwanza. Ni vigezo vipi vilivyokamilishwa ilihali ikiwa Dodoma iwe nongwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakata niseme tu Waheshimiwa Wabunge, mimi nimewaomba na Wabunge wa Dodoma tunawaomba wenzetu Wabunge muunge mkono azimio hili kumpongeza Mheshimiwa Rais na yale yote mliyoyasema Waheshimiwa Wabunge na kwenye maazimio

tumesema; kwenye Azimio namba mbili tumeiomba Serikali kuongeza rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi miundombinu mbalimbali ili kukidhi vigezo hivyo ambavyo vina upungufu. Kwa sababu hakuna kitu ambacho kimekamilika hata katika miji mingine ambayo imetangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa Dodoma kwa sababu ya hadhi yake ya Makao Makuu ambayo hakuna anayebisha hata mmoja, basi hivi vyote tunaamini vitakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie tena kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, nasi wananchi wa Dodoma na kwa niaba ya wenzangu Wabunge wa Dodoma, hususan Mheshimiwa Spika ambaye ameruhusu Azimio liweze kusomwa, tunasema hivi, zawadi yetu kwa Mheshimiwa Rais Magufuli itakuwa ni kubwa mwaka 2020, ndiyo ahadi tunayoitoa kwake. Tunamshukuru kwa haya makubwa anayoifanyia Dodoma, tunamshukuru kwa kututoa gizani na sasa ametuweka kwenye mwanga. Ninawaomba kwa sababu na nyie Waheshimiwa Wabunge wote ni sehemu ya maendeleo ya Dodoma, mtuunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja tena. *(Makofi)*

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono kwa asilimia kubwa sana. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Uamuzi wake wa Kuundeleza Mji wa Dodoma na Kuupa Hadhi ya Jiji liliridhiwa na Bunge)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Azimio limepita kwa asilimia zote. Wale ambao wamezungumza tofauti, nafikiri wanakazia swaumu tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo muhimu sana; tangazo hili linatoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa kesho ni siku ya Bajeti, tarehe 14 Juni. Asubuhi baada ya maswali kutakuwa na Mpango wa Serikali, baada ya Mpango wa Serikali, Bajeti itasomwa jioni saa 10.00.

Kutakuwa na wageni mbalimbali walioalikwa na Bunge, nchi rafiki, mabalozi, *donors* na wageni wa kitaifa. Wabunge wote wanapewa taarifa kwamba hakuna Mbunge yeyote kukosa kuwepo kesho kwa shughuli hii muhimu ya kitaifa.

Narudia tena Wabunge wote wanatakiwa kuwepo kesho. *(Makofi)*

Baada ya maneno haya, nakushukuru sana mtoa hoja na wachangiaji wote. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 5.37 asubuhi Bunge liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 14 Juni, 2018 saa Tatu Asubuhi)